# KISWAHILI

# DARASA LA TANO

**LUGHA**

**MUHULA WA KWANZA**

**SURA YA KWANZA**

KUSOMA : UFAHAMU

Siri tatu

- Kuchambua picha
- Kuchambua na kuorodhesha msamiati
- Kutunga sentensi ukitumia msamiati
- Kusoma ufahamu kwa vikundi na kwa sauti, mmojammoja kimyakimya
- Kuchambua na kueleza msamiati husika

  Tathmini: mufti uk 3 (1-10)

**SARUFI: NGELI**

Ngeli ya A-WA

Nomino huchukua kiambishi A kwa umoja na WA kwa wingi

Huwa ni nomino za makundi ya:-

a. Wanyama:
    - Ng'ombe
    - Ngamia
    - Punda
    - Chura

b. Wadudu:
    - Kipepeo
    - Nondo
    - Nyigu
    - Siafu
c. Nyuni/ ngege:
    - Ninga
    - Kuku
    - Kanga
    - Korongo
    - Mwewe
d. Wanadamu:
    - Daktari
    - Mtu
    - Mwalimu
    - Nesi
    - Kinara
    - Bawabu
e. Samaki
    - Mamba
    - Pono
    - Mkizi
f. Malaika
g. Mungu
h. Shetani

i. Maiti

**Mifano ya sentensi**

a. Mtume amewasili    mitume wamewasili
b. Chura anaruka    vyura wanaruka
c. Bawabu analinda lango    mabawabu wanalinda malango

- Tathmini: mufti uk 6
- Kurunzi uk 4
- Kkd uk

**MSAMIATI: nyumbani**

Sebuleni

Sebuleni ni mahali pa kukaa katika nyumba .

Ni chumba cha kupumzikia, kuongea na kupokea wageni

Huwa na vifaa kama:

- ✓ Kochi    makochi
- ✓ Runinga    runinga
- ✓ Takia    matakia
- ✓ Kinanda    vinanda
- ✓ Meza    meza
- ✓ Redio    redio
- ✓ Simu    simu
- ✓ Rafu    rafu
- ✓ Dari    madari
- ✓ Sofa    sofa
- ✓ Picha    picha
- ✓ Shubaka    mashubaka
- ✓ Meza    meza
- ✓ Kiti    viti

Kusoma mifano

Kuchambua picha

Tathmini:    mufti uk 7

Kkd uk 9

Kurunzi uk 1-3

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Shairi: elimu ndiyo maisha**

- Shairi ni wimbo wa kiswahili
- Malenga ni anayetunga shairi
- Manju ni anayeghani mashairi
- Mshororo ni mstari katika ubeti
- Ubeti ni kifungu cha mishororo
- Kibwagizo ni mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa
- Tarbia ni shairi la mishororo mine

- ✓ Kuchambua msamiati
- ✓ Kutunga sentensi kutumia msamiati
- ✓ Kughani shairi kwa sauti katika vikundi

Tathmini: mufti uk 8

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

<u>Maadili</u>

Maadili ni mwenendo mwema , mambo ya haki au mafundisho yanayozingatia adabu na tabia njema

Kujadiliana

Kusoma maelezo

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

Tathmini: mufti uk 8 – 9

Kurunzi uk 34

Kkd uk 42

## SURA YA PILI

**KUSOMA :ufahamu**

Kuchambua picha

Kuchambua na kueleza maana ya msamiati

Kutunga sentensi wakitumia msamiati

Kusoma kifungu

Kuchambua msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 11 – 12

**SARUFI**

**Ngeli ya U – I**

Hili ni kundi la mimea, miti na nomino zingine za kawaida

Nomino huchukua M, MU, au MW umoja na MI kwa wingi

**Mimea**

- Mti utakatwa miti itakatwa
- Mchungwa una machungwa michungwa ina matunda
- Mkahawa umefungewa mikahawa imefungwa

**Baadhi ya sehemu za mwili**

- Mkono umevunjika mikono imevunjika
- Mguu unauma miguu inauma

- Mgongo umenyooka migongi imenyooka
- Mfupa umekua mifupa imekua

**Nomino zingine**

- Mswaki ulinunuliwa miswaki ilinunuliwa
- Mlima una theluji milima ina theluji
- Msitu utafyekwa
- Mfuko umeraruka
- Mwezi umeisha

**MSAMIATI**

Salamu na maneno ya adabu

Salamu ni ujumbe wa kujuliana hali baina ya watu

Maneno ya adabu huzingatia maadili

**Mfano**

Hujambo? Sijambo

Mwambaje? hatuna la kuamba

U hali gani? Njema/ nzuri

U mzima? Ni mzima

**Adabu na heshima**

- ✓ Pole
- ✓ Tafadhali
- ✓ Samahani
- ✓ Simile
- ✓ Niwie radhi
- ✓ Ugua pole
- ✓ Mjamzito
- ✓ Jifungue
- ✓ Endesha

Tathmini: mufti uk 16

Kkd uk 2

Kurunzi uk 7 -8

**KUSOMA**

**Matamshi ya dh na th**

- ❖ Kutamka silabi dh na th
- ❖ Kutaja baadhi ya maneno
- ❖ Kuyaorodhesha ubaoni na kuwashirikisha kutamka
- ❖ Kusoma mifano
- ❖ Kuchambua na kueleza maana ya maneno
- ❖ Kusoma sentensi

Tathmini: mufti uk 16

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

Hadithi na mafumbo

Hadithi ni utungo wenye wahusika na hutoa matukio yaliyotendeka

Fumbo ni swali la chemshabongo linalohitaji utumizi wa ubongo kungamua jawabu

Kutamba hadithi

Kutoa mafumbo na majibu

Mfano

- Yai moja huive likicchemshwa kwa dakika tatu. Je, mayai matano yatachukua dakika ngapi?
- Mama wawili na wana wawili walienda dukani wakaagiza chupa tatu za soda. Kila mmoja alinywa yake bila kugawana. Je, haya yaliwezekanaje?

Tathmini: mufti uk 17

Kkd uk 111

Kurunzi uk 96

**SURA YA TATU**

**KUSOMA: UFAHAMU**

Yaya juha

Kuchambua picha

Kuchambua na kueleza msamiati

Kutunga sentensi kutumia msamiati

Kusoma ufahamu

Kuchambua msamiati ibuka na kueleza maana

Tathmini: mufti uk 20

**SARUFI**

Ngeli ya LI- YA

- Huchukua makundi mawili ya nomino
- Nomino za kawaida zinazoanza kwa MA au ME kwa wingi
- Nomino katika hali ya ukubwa

**Za kawaida**

| | | |
|---|---|---|
| Shati | Darasa | Yai |
| Jino | Zulia | Umbo |
| Jiko | Kochi | Gani |
| Jani | Boma | Kabati |
| Jiwe | Wingu | Lango |
| Sanduku | Duka | Koti |
| Dawati | Ua | Soko |

**Ukubwa**

| | | |
|---|---|---|
| Jitu | Buzi | Joka |
| Guu | Gombe | Jumba |
| Jumba | Toto | Jichwa |
| Jitu | Dume | Domo |

Tathmini: mufti uk 21

Kurunzi uk 3

**MSAMIATI**

MAVAZI

Vitu vinavyovaliwa mwilini kwa madhumuni ya kufunika uchi

Kuna mavazi tofauti kv ya waume, wake, watoto na shughuli maalum

**Mfano**

| | | |
|---|---|---|
| Surupwenye/bwelasuti | Sindiria | Suruali |
| Sufi | Sare | Bombo/kaptura |
| Joho | Aproni | Buibui |
| Tarbushi | Kidotia | Kanzu |
| Kitenge | Kabuti | Saruni |
| Jezi | Shati | Tai |
| Rinda | Bulibuli | Shimizi |
| Koti | Fulana | |
| Kocho | Viatu | |

Tathmini: mufti uk 33

Kkd uk 14

Kurunzi uk 12

**KUSOMA**

Matamshi ya **sh**, **s** na **z**

Kuorodhesha sauti sh, s na z

Kutamka barabara

Kutaja baadhi ya majina na kuorodhesha ubaoni

**Mifano**

| | | |
|---|---|---|
| Mazishi | Songeza | Masizi |
| Kusinzia | Uzushi | Sambaza |

| | | |
|---|---|---|
| Sababisha | Sindikiza | Zalisha |
| Starehe | Zorotesha | Zungusha |

Tathmini: mufti uk 24

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

- Sentensi zenye majina , vivumishi, vitenzi na vielezi
- Jina/ nomino ni jina la kitu , mtu, mahali au hali
- Kivumishi ni neno linaloeleza nomino
- Kitenzi ni neno linaloonyesha kitendo
- Kielezi ni neno linaloeleza kitenzi

**Mifano**

1. Mwanafunzi mdogo ameanguka vibaya
2. Mtu mzuri amezungumza taratibu
3. Mtoto mkorofi ameadhibiwa vibaya
4. Chura mzee anatembea polepole
5. Kiatu change kinangara zaidi

Tunga sentensi saba

Tathmini: mufti uk 28

**SURA YA NNE**

**KUSOMA: UFAHAMU**

Kilichomtoa kanga manyoya

- Kuchambua picha
- Kuchambua na kueleza msamiati

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

- Kutunga sentensi kutumia msamiati
- Kusoma ufahamu
- Kuchambua msamiati ibuka na kutungia sentensi

Tathmini: mufti uk 28

SARUFI

Viulizi ---------pi? Na ---------ngapi?

Kiulizi ni neon la kuulizia kutaka kujua baina ya vitu vingi(-pi?)

Ngapi? Kiulizi cha kutaka kujua zaidi

Mfano

| | | | |
|---|---|---|---|
| A<br>WA | Yu<br>Wa/we | Yupi<br>Wapi/wepi | -----------<br>Wangapi |
| KI<br>VI | Ki<br>Vi | Kipi<br>Vipi | --------------<br>Vingapi |
| LI<br>YA | Li<br>Ya | Li[pi<br>Yapi | ---------------<br>Mangapi |

Tanbihi: kiulizi ngapi? Hakitumiki kwa umoja

Tathmini: mufti uk 29-30

Kurunzi uk 39-41

Kkd uk 13

**MSAMIATI**

**Hospitali**

- Hospitali ni mahali ambapo watu wanaougua huenda kupata matibabu

- Zahanati, kliniki, kituo cha afya ni hospitali ndogo ya kutibia magonjwa mbalimbali
- Anayewatibu wagonjwa ni daktari, tabibu au mganga
- Anasaidiwa na muuguzi, nesi
- Kuna vyumba kama wodi, mochari, thieta nk

**Vifaa ni kv:**

Kitanda

Bandeji

Uyoka

Maabara

Ambulensi

Sindano

Tembe

Kipimajoto

Kipimamwili

Dawa

Machela

- Kutazama michoro/ vifaa na kuvitaja
- Kusoma maelezo
- Kutunga sentensi

Tathmini: mufti uk 31

Kurunzi uk 38

Kkd uk 30

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Sauti ya ch, j na sh**

- Kusoma matamshi ch, j n ash
- Kutoa mifano ya maneno yenye sauti hizo
- Kusoma jedwali lenye mifano ya maneno hayo
- Kutoa maana ya baadhi ya maneno
- Kutunga sentensi kutumia maneno hayo

Tathmini :mufti uk 31-32

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

**Vitendawili**

Kitendawili ni swali la chemshabongo ambalo mtu huwaza kabla ya kutoa jibu

Huwa na mtegaji na mtegewa

Huwa na mwanzo maalum

Mtegaji: kitendawili

Mtegewa: tega

Aliyetegewa asipopata hupewa mji

**Mifano**

1. Chukua nafasi tumfinye mshenzi: sima/ kula ugali
2. Nuyumbani mwangu mna shetanianayeyanywa maji yangu: utambi wa taa
3. Chakula kikuu cha watoto: usingizi
4. Mombasa kwametameta: harusi
5. Mzee wangu ana koti la chuma: kombe

Tathmini: kurunzi uk 65

Kkd uk 20-21

**SURA YA TANO**

**KUSOMA:ufahamu**

- Kuchambua picha
- Kuchambua msamiati na kueleza maana
- Kutunga sentensi kutumia msamiati
- Kushiriki usomaji
- Kuchambua msamiati ibuka , kueleza maana na kutunga sentensi

Tathmini: mufti uk 34-35

**SARUFI**

**Kirejeshi amba**

Kirejeshi amba hutumika kama kitenzi kinachorejelea au kinachorudia jina, kitenda au kitendwa katika neon la kitenzi

Huchukua viambishi vya ngeli husika

**Mifano**

1. Mtu ambaye alilima watu ambao walilima
2. Mti ambao ulianguka miti ambayo ilianguka
3. Jembe ambalo lilivunjwa majembe ambnayo yalivunjwa
4. Maji ambayo yalimwagika maji ambayo yalimwagika

Tathmini: mufti uk 36

Kkd uk 57-58

Kurunzi uk 53-54

**MSAMIATI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**Akisami**

Akisami ni hesabu au tarakimu zinazoonyesha sehemu ya ujumla au ya kitu kizima

Baadhi ya akisami

- ✓ Nusu
- ✓ Theluthi
- ✓ Robo
- ✓ Humusi/ humsi
- ✓ Sudusi
- ✓ Subui
- ✓ Thumni
- ✓ Tusui
- ✓ Ushuru
- ✓ Subui tatu

Tathmini: mufti uk 37

Kkd uk 49 -50

Kurunzi uk 126-128

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Lugha mseto na vihasho**

Kueleza msamiati husika mfano: shuleni

Kuwahimiza kutoa majibu sahihi ili kuleta maana iliyokusudiwa

Kuwaelekeza kusoma bilakujaza mapengo

Kueleza ngeli za maneno yaliyotumika

Kujadili maendelezo ya majibu na nyakati zilizotumika

Kuwapa furtsa kuandika madaftarini na kutoa majibu

Tathmini: mufti uk 37

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

Shairi: elimu

Shairi ni wimbo wa Kiswahili

Malenga anayetunga mashairi

Manju anayeghani mashairi

Sentensi katika shairi ni mshororo

Ubeti ni kifungu cha mishororo

Kusoma shairi

Kughani katika vikundi kwa kujibizana

Kuchambua na kueleza msamiati husika

Wajibu maswali ya kauli

Tathmini: kkd uk 18

**SURA YA SITA**

**KUSOMA:ufahamu**

**Mzigo wa siri**

Kujadili mada na kueleza maana

Kushiriki usomaji kwa zamu

Kuchasmbua na kueleza msamiati uliotumika

Kutunga sentensi wakitumia msamiati huo

Kuchambua na kueleza maana ya msamiati ibuka

Kutunga sentensi wakitumia msamiati ibuka

Watoe visa vyao kwa zamu

Tathmini: mufti uk 41

**SARUFI**

**Ngeli ya YA-YA**

Kundi hili ni la majina ya vitu vya kawaida vya mshikamano ambavyo huanza kwa silabi MA kwa umoja na kwa wingi

Nomino hazina wingi

**Mifano**

- Maji
- Mate
- Maradhi
- Maziwa
- Mali
- Manukato
- Makala
- Mauti
- Mazingira
- Maendeleo
- Mazishi
- Maarifa
- Majira
- Mafuta
- Marashi

Kuwashirikisha kutaja ngeli

Mwalimu aeleze ngeli ya YA-YA

Watoe mifano ya nomino katika ngeli hii

Wasome mifano ya majina na sentensi vitabuni

Watunge sentensi kutumia majina

Tathmini: mufti uk 42

**MSAMIATI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**Mimea na mazao**

Mmea ni kitu kiotacho ardhini kutokana na mbegu

Mazao ni matunda yanayotokana na mmea

Mche: mmea mdogo

**Mifano**

- Mwembe embe
- Mpera pera
- Mchungwa chungwa
- Mparachichi parachichi
- Mpareto pareto
- Mkahawa kahawa
- Mtufaha tufaha
- Mzabibu zabibu
- Mkwaju ukwaju
- Mtende tende
- Mpapai papai
- Mgomba ndizi
- Mnazi nazi
- Mpunga mchele
- Mboga boga
- Mtikiti tikiti
- Mlimau limau
- Mhogo mhogo/kisamvu

Kuwashilikisha kutaja baadhi ya mimea na mazao

Kuwapeleka kundini kubainisha baadhi ya mimea

Kusoma mifano ya mimea na mazao

Tathmini: mufti uk 43

Kurunzi uk 19-20

Kkd uk 34-35

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Matamshi ya R na L**

Kuwashirikisha kutamka sauti r na l

Kuwashirikisha kutoa mifano ya majina yenye sauti r na l na kuorodhesha ubaoni

Kuwaelekeza kutunga sentensi sahihi

Kuwaelekeza kusoma miofano ya nomino na vitenzi na sentensi

Tathmini: mufti uk 43-44

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

**Misemo**

Misemo huundwa kwa kitenzi na nomino

Huwa na maana maalum

Maana huwa fiche

**Mifano**

- Kula chumvi zeeka
- Kula mwande pata taabu

- Ona haya fedheheka, aibika
- Piga mbio kimbia
- Chana mbuga kimbia
- Lalia mate lala njaa
- Kata kamba kufa
- Mkono birika mchoyo
- N'goa nanga anz a safari

Kueleza maana ya semi

Kutoa mifano na kueleza maana

Kuwashirikisha kusoma mifano

Tathmini: mufti uk 111-112

Kurunzu uk 121

Kkd uk 25

**SURA YA SABA**

**KUSOMA: ufahamu**

Nyama nzuri na nyama mbaya kuliko zote(1)

- Kuchambua picha
- Kuchambua mada
- Kushiriki usomaji, kwa zamu
- Kueleza maana ya msamiati
- Kuchambua na kueleza maana ya msamiati ibuka
- Kutunga sentensi kutumia msamiati

Tathmini: mufti uk 47-48

**SARUFI**

**Vivumishi vya pekee enye na enyewe**

Kivumishi ni neon linalotoa maelezo kuhusu nomino au jina

Enye ni kivumishi cha umilikaji. Huonyesha kinachozungumziwa kina

Enyewe huonyesha binafsi au bila kuandamana na mwengine au kingine

**Mfano**

Mtu mwenye nundu

Mvulana mwenye lalamu

Kiranja mwenyewe afute ubao

Msichana mwenyewe alilima

Kueleza maana ya kivumishi enye na enyewe

Kutoa mifano ya sentensi

Kusoma mifano na jedwali

Tathmini: mufti uk 48-50

Kkd uk 48 na 76-77

Kurunzi uk 21 -22

**MSAMIATI**

**MALIPO**

Malipo ni kitu au pesa apatazo mtu kwa kugharamia shughuli au jukumu Fulani

**Mfano**

- Nauli
- Kiingilio
- Ujira
- Rushwa/ kadhongo

- Arbuni
- Ada
- Karo
- Mahari
- Risimu
- Mshahara
- Fidia
- Faini
- Zawadi
- Kiokosi
- Tuzo

Kuwashirikisha kueleza maana ya malipo

Kuwashirikisha kujibu maswali ya kauli

Wasome mifano vitabuni huku mwalimu akieleza maana

Kuwashirikisha kutunga sentensi kutokana na msamiati wa malipo waliosoma

Tathmini: mufti uk 50-51

Kkd uk 93-94

Kurunzi uk 138-139

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Matamshi ya sauti b na mb**

Kuwaongoza kusoma na kutamka sauti b na mb

Kuwashirikisha kutaja baadhi ya majina yenye sauti hizo na kuorodhesha ubaoni

Kuwashirikisha kusoma na kutamka kwa sauti

Kuwaongoza kusoma mifano ya majina na sentensi

Kuwapa fursa kutunga sentensi wakitumia sauti b na mb

Tathmini: mufti uk 51-52

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

**Mafumbo**

Fumbo ni swali la chemshabongo

Huhitaji kufikilia ili kupata jibu

Anayefumba hujaribu kuonyesha werevu

**Mfano**

Gari la umeme lilikuwa likisafirisha mtu kwa basi kwenda kusini. Upepo ulikuwa ukiruma kutoka kaskazini. Je moshi wa gari hilo ulikuwa ukielekea upande gani?

Jibu: gari la umeme halitoi moshi

Kuwashirikisha kutoa maana ya mafumbo

Kuwapa fursa kutoa mifano na jibu

Kuwaongoza kusoma mifano na kutoa majibu

Tathmini: mufti uk 17

Kkd uk 111

Kurunzi uk 96-97

**SURA YA NANE**

**KUSOMA: ufahamu**

Bwawa la jinni wa nidhamu

Kuchambua mada

Kuwaongoza kusoma kwa sauti katika vikundi kasha kimyakimya mmojammoja

Kuwaongoza kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi kutumia msamiati

Kuchambua msamiati ibuka na kuutungia sentensi

Tathmini: mufti uk 55

**SARUFI**

**Vivumishio vya pekee ote na oote**

Kueleza maana ya kivumishi

Kurejelea vivumishi vya pekee enye na enyewe

Ote: kivumishi cha jumla au pamoja ambacho hurejelea majina bila kuyagawanya au kutenganisha

Oote: kivumishi cha kuonyesha kati ye wengi au vingi lakini si wote wala vyote kwa pamoja

Huonyesha baadhi tu

**Mfano**

| | | |
|---|---|---|
| A<br><br>Wa | Wote<br><br>Wote | Yoyote<br><br>Wowote |
| Ki<br><br>vi | Chote<br><br>Vyote | Chochote<br><br>Vyovyote |
| Li<br><br>ya | Lote<br><br>yote | Lolote<br><br>Yoyote |

Kuwashirikisha kusoma jedwali

Tathmini: kkd uk 18-19,53-54, 71-72

Mufti uk 55-56

Kurunzi uk

**MSAMIATI**

**Ukoo**

Ukoo ni neon linalotumiwa kumaanisha kikundi cha watu wanaotokana na nasaba, jamaa au mlango mmoja

Kuwauliza kutaja majina ya watu kutoka familia zao

**Mifano**

| | |
|---|---|
| Baba | Mnuna |
| Mama/nina | Ndugu |
| Shangazi | Kaka |
| Mjomba | Bintiamu |
| Amu/ ami | Shemeji |
| Halati/ hale | Wifi |
| Nyanya/ bibi | Mama wa kambo |

Kuwashirikisha kueleza uhusiano uliopo baina yao na watu waliowataja

Wasome maelezo vitabuni huku mwalimu akitoa maelezo

Watunge sentensi wakitumia msamiati huo

Tathmini: mufti uk 57-59

Kkd uk 45

Kurunzi uk 29-30

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Matamshi gh na h**

Kuwaongoza kutamka sauti gh na h

Kuwashirikisha kutoa mifano yenye sauti gh na h na kuyaorodhesha ubaoni

Kuwashirikisha kuyasoma na kuyatamka kwa ufasaha

Kuwaongoza kusoma mifano ya maneno na sentensi vitabuni

Kuwapa fursa kutunga sentensi zenye sauti gh na h

Tathmini: mufti uk 59-60

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

**HADITHI**

Kuwashirikisha kueleza maana ya hadithi

Kuwapa fursa kutamba hadithi zao mbele ya wenzao kwa zamu

Mwalimu kutoa hadithi moja

Kuwashirikisha kusoma hadithi

Kuwapa fursa kutoa maelezo kwa muhtasari waliojifunza

Kuchambua msamiati na kutunga sentensi

Tathmini: kurunzi uk 33-34

**SURA YA TISA**

**KUSOMA: ufahamu**

Mke wa mvuvi(1)

Kuchambua picha vitabuni

Kuchambua na kueleza mada

Kushiriki usomaji kwa sauti kama darasa, vikundi

Kuchambua na kueleza maana ya msamiati

Kusoma kimyakimya mmojammoja

Kutunga sentensi wakitumia msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 61-63

**SARUFI**

**Ngeli ya U-ZI**

Majina huanza kwa namna tofauti

**U-NY**

Uta nyuta

Uma nyuma

**U-ND**

Ulimi ndimi

Udevu ndevu

**U-MB**

Ubawa mbawa

Ubavu mbavu

**W-NY**

Wimbo nyimbo

Wavu nyavu

**U-***

Ufunguo funguo

Unywlw nywele

Ufagio fagio

Tanbihi: U-* u huondoshwa kwa wingi

Kuongoza kutaja ngeli wazijuazo

Mwalimu aeleze ngeli ya U-ZI

Awashirikishe wanafunzi kutaja baadhi ya majina katika ngeli hii

Kuwashirikisha kutunga sentensi katika ngeli ya U-ZI

Kuwashirikisha kutunga sentensi katika ngeli ya U-ZI Katika umoja na wingi

Kuwapa fursa kusoma mifano ya nomino na sentensi

Tathmini: mufti uk 63-64

MSAMIATI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Viungo vya nje ya mwili**

Mwalimu awaongoze kuimba wimbo 'naskia kichwa'

Waimbe wakiguza baadhi ya viungo vya nje vya mwili

Kuwaongoza kwa kutaja viungo zaidi na kuvigusa

Kutunga sentensi wakitumia majina ya sehemu za nje za mwili

Kuwaongoza kutazama michoro na kusoma maelezo

Kuwaongoza kuchora na kutaja / kuonyesha sehemu za nje za mwili

Tathmini: mufti uk 63-64

Kkd uk 39-40

Kurunzi uk 50-52

KUSOMA NA KUANDIKA

**Tarakimu**

Kuwaongoza kutaja baadhi ya tarakimu kutoka elfu kumi hadi laki moja

Kuwaongoza kutunga sentensi wakizingatia ngeli tofauti za nomiono

Kuwashirikisha kusoma maelezo

Tathmini: uk 54

KUSIKILIZA NA KUONGEA

**Barua ya kirafiki**

Kuwaongoza kueleza baadhi ya sehemu za barua ya kirafiki

Nazo ni:

- Anwani ya mwandishi na tarehe
- Anayeandikiwa
- Mwanzo/ salamu
- Utangulizi
- Kiwiliwili/ mtiririko
- Kimalizio/ wasalaam
- Mwandishi

Kuwashirikisha kusoma mfano wa barua ulioandikwa katika ukurasa wa 67

Kuchambua msamiati uliotumika

Kuwashirikisha kutunga sentensi wakitumia msamiati

Tathmini: mufti uk 67

**SURA YA KUMI**

**KUSOMA: ufahamu**

Usiniajiri nataka kusoma

Kuchambua picha

Kuchambua mada

Kuwashirikisha kusoma kwa sauti, kasha kimyakimya katika vikundi na kibinafsi

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kuwaongoza kutunga sentensi wakitumia msamiati huo

Kuchambua na kueleza maana ya msamiati ibuka

Kutungia msamiati ibuka sentensi

**SARUFI**

**Vikanushi**

Kikanushi ni kiambishi kinachoonyesha kukanusha katika sarufi

Kukanusha ni kukataa au kupinga

Kuwashirikisha kutaja nafsi zote tatu kwa umoja na kwa wingi

Kuwashirikisha kutaja nyakati mbalimbali

Kuwaongoza kutaja viwakilishi nafsi na ukanusho wake

Mfano

| nafsi | Viwakilishi nafsi | Vikanushi |
|---|---|---|
| Mimi | Ni | Si |
| Sisi | Tu | Hatu |
| Wewe | U | Hu |
| Nyinyi | M | Ham |
| Yeye | A | Ha |
| wao | wa | Hawa |

Kuwashirikisha kusoma mifano ya sentensi

Tathmini: mufti uk 72-73

Kkd uk 8

**MSAMIATI**

**Tarakimu**

Tarakimu ni alama ya hesabu inayoonyesha idadi au nambari ya vitu Fulani

Kumi elfu na moja hadi laki moja: 10001-100000

Kuwaongoza kutaja baadhi ya tarakimu kati ya kumi elfu na moja na laki moja

Kuwashirikisha kutunga sentensi wakizingatia ngeli tofauti pamoja na tarakimu walizotaja

Kuwaelekeza kusoma maelezo vitabuni

Tathmini: mufti uk 73-74

Kurunzi uk 61-62

**KUSOMA NA KUANDIKA**

**Matamshi g na k**

Kuwaongoza kusoma na kutamka sauti k na g

Kuwaongoza kutoa mifano ya majina yenye sauti g na k na kuyaorodhesha kwenye ubao

Kuwaelekeza kuyasoma kwa sauti katika vikundi

Kuwashirikisha kusoma jozi za maneno waliyopewa vitabuni

Kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia jozi za maneno hayo

Tathmini: mufti uk 75

**KUSIKILIZA NA KUONGEA**

**Methali**

Methali ni usemi unaotumika kuelimisha na kuonya

Kuwashirikisha kutaja mifano ya methali

Kuwaelekeza kutoa maana fiche ya baadhi za methali

Kuwashirikisha kusoma mifano na maana vitabunio

**Mfano**

- Adui mpende
- Bendera hufuata upepo
- Damu ni nzito kuliko maji
- Bandu bandu huisha gogo
- Maji yakimwagika hayazoleki

- Dua la kuku halimpati mwewe
- Mtegemea nundu haachi kunona

Tathmini: kkd uk 78

Kurunzi uk 122-123

Mufti uk 79-80

MUHULA WA KWANZA INSHA

## UMUHIMU WA MITI

Mti ni mmea mwenye shina, matawi, mizizi, maua, tenzu na matunda

Mti mdogo ni mche-miche

Mti hutokana na mbegu

Umuhimu

Ni makao ya hayawani wa porini na nyuni

Hutupa dawa za kienyeji/ kiasili

Hutumika kutengeneza karatasi

Hutupa makaa na kuni-upishi

Hutupa mbao-seremala huunda samani/fanicha

Hutupa matunda-protini-hutukinga dhidi ya maradhi, magonjwa

Hutengeneza nyua za kuwekea mipaka

Miti huzuia mmomonyoko wa udongo

Hutupa kivuli wakati wa kiangazi

Huvuta mvua

Hutukinga kutokana na upepo mkali

Vyakula vya wanyama-majani, matunda

Chanzo cha mito na chemichemi za maji

Hutupa vikingi na fito-ujenzi

Hutumika kutengeneza gundi

Huwa kivuto cha watalii

## Methali

Penye miti hapana wajenzi

Mti ukifa shinale na tenzuze hukauka

Mtaka cha mvunguni sharti ainame

Maji ni uhau

Mti mkuu ukigwa wanadege huyumba

**Msamiati**

Ukikata mmoja panda miwili au zaidi

Miti ina umuhimu chungu mzima/teletele

Tusikate miti ovyo ovyo ardhi itakuwa jangwa

Miti mingi pamoja ni msitu, mwitu, pori

Miti mingine ni mirefuja mlingoti ilhali mingine huwa mifupi mithili ya nyundo

Matunda matamu kamauki/ asali/

Maua meupe pepepe

**BARUA YA KIRAFIKI**

Huandikiwa watu wa nasaba moja au rafiki

Mwandishi na mwandikiwa huwa na uhusiano wa karibu

Huwa na sehemu tano kuu

**Anwani**

Huwa moja ya mwandishi

Huwa na:

- jina la mwandishi
- Sanduku la posta
- Mji

**Tarehe**

Huandikwa wa namna tofauti

- 8.4.15
- 8/4/2015
- 8-4-2015
- Aprili 8, 2015

**Utangulizi**

Humlenga mwandikiwa

Mfano

Kwa baba mpendwa

Kwa sahibu mpendwa

Kwa mpendwa otongolo

**Mwili/ kiwiliwili**

Hutoa lengo la mwandishi kwa mwandikiwa yaani ujumbe hutolewa

Hutangulia kwa kujuliana hali

Lengo hufuata

Mwisho hutuma salamu kwa jamaa au marafiki kupitia mwandikiwa

**Wasalaam/ maagano**

Mwandishi humuaga mwandikiwa

Huonyesha uhusiano uliopo baina ya mwandishi na mwandikiwa

**Mfano**

Ni mimi pumzi wa moyo wako

Ni mwanao mpendwa

Mamako mpendwa

Jina la mwandishi hufuata maagano

Ni mimi mwanao mpendwa

john kimani

**muundo**

Anwani

Tarehe

utangulizi

mwili/ kiwiliwili

maagano/wasalaa
m

**MSAMIATI**

Pokea salamu sufufu/ tele/ telele kama

Mchanga baharini

Nywele kichwani

Nyota angani

Wana wa ibrahimu

Mimi mzima kama kigongo

Imara kama chuma cha pua

Barua ni waraka/ nyaraka

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Mvumilivu hula mbivu

Mtaka cha mvunguni sharti ainame

**HADITHI**

Pia huitwa ngano au hekaya

Huwa na utangulizi maalum

**Mfano**

- Paukwa! Pakawa. Hapo zamani za kale…………….
- Hadithi hadithi! Hadithi njoo. Hapo kale………….
- Hapo miaka na mikaka…………………………
- Hapo jadi na jadudi…………………………….
- Hapo zamani za kale…………………………………………

Ni muhimu kutumia mapambo tofauti

**Mfano**

**Tashbihi**

- Mjanja kama sungura
- Mkali kama samba
- Chungu kama shubiri(ladha)
- Mweusi kama makaa/ lami/ mpingo/ kizimwili
- Mfupi kama nyundo/ mbilikimo
- Chafu kama fuko
- Nuka kama beberu/ kidonda
- Iga kama kasuku

**Tanakari za sauti**

- Cheka kwa kwa kwa
- Lia kwi kwi kwi
- Anguka majini chubwi
- Anguka sakafuni pu
- Anguka matopeni tapwi
- Anguka mchangani tifu
- Shiba ndi
- Lala/ kufa fo fo fo
- Nyamaza ji
- Maliza fyu
- Tukia tuli

**Misemo**

- Angua kicheko
- Angua kilio
- Chana mbuga
- Pata nafuu
- Piga mbio
- Shtaki njaa
- Enda jongomeo
- Lalia mate
- Ona haya

**SHEREHE NILIYOSHUHUDIA**

Sherehe ni tukio au shamrashamra za furaha

Sherehe huleta halaiki ya watu pamoja

**Mifano**

- Harusi/ arusi
- Kuzaliwa kwa mtu
- Mazishi-sherehe ya huzuni
- Krismasi
- Siku za kitaifa: mashujaa, jamhuri, madaraka
- Mahafali
- Kusherehekea matokeo ya mtihani

**Msamiati**

Tuliamka alfajiri na mapema

Nilioga kwa maji baridi barafu kando/ vuguvugu/ fufutende

Nilivalia nguo mpya/ nadhifu/ zilizopigwa pasi zikanyooka twaa

Nina aliandika meza kwa mahamri, si chai, si mkate, si mandazi, si mayai, si maziwa

Niliongoza sala za asubuhi kumshukuru jalali/ mola

Tulikila kiamshakinywa/ kisebeho taratibu

Sherehe yenyewe

**Methali**

- Mvumilivu hula mbivu
- Chanda chema huvikwa pete
- Polepole ndio mwendo
- Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
- Mkono mmoja haulei mwana
- Subira huvuta heri

**Tashbihi**

- Kishuka kilikuwa kitamu kama halua
- Pendana kama chanda na pete
- Fanana kama shilingi kwa ya pili
- Adimika kama barafu ya kukaanga
- Yeyuka kama barafu kwa moto

**BARUA RASMI**

Pia huitwa barua ya kiofisi

Huandikwa kwa nia ya kuomba nafasi ya shule

Huwa na sehemu sita

- Anwani ya mwandishi na tarehe
- Anwani ya mwandikiwa
- Maamkizi
- Mtajo
- Mwili
- Tamati

**Anwani ya mwandishi na tarehe**

Huandikwa kwa herufi kubwa upande wa kulia

Tarehe hufuata

**Anwani ya anayeandikiwa**

Huandikwa kushoto chini ya anwani ya mwandishi

**Maamkizi**

Huandikwa chini ya anwani baada ya kuruka mstari

**Mtajo**

Ni muhtasari wa lengo kuu

Kama vile: KUH: kuhusu

KUS: kusudio

MINT: mintarafu

YAH: yahusu

KUMB: kumbukumbu

**Mwili**

Hutoa lengo la kuandika

**Tamati**

Huandikwa:

Wako mtiifu

Wako mwaminifu

| |
|---|
| ANWANI YA MWANDISHI<br><br><br>TAREHE |

| |
|---|
| ANWANI YA MWANDIKIWA |

| |
|---|
| MAAMKIZI |

| |
|---|
| MTAJO WA BARUA |

| MWILI WA BARUA |
|---|

| MWISHO<br>SAINI<br>MAJINA YA MWANDISHI |
|---|

**MKASA WA MOTO**

Mkasa huu huwa wa huzuni na huleta maafa na hasara tele

Chanzo cha mota

Jiko la makaa

Mishumaa

Kucheza na viberiti

Kibatari

Vijinga vya kuni

Umeme

Mpangilio/ hatua

Nyumba ikateketea

Mali nyingi kuteketea

Hasara kubwa kutokea

Tulibaki nyumbani na ndugu yangu

Wazazi walienda safarini

Tuliamka na kuwaaga wavyele

Tulila kiamshakinywa kitamu ja uki

Tulitazama runinga hadi saa tano

Tulitoka kucheza na marafiki

Rafiki akaona moshi ukifuka toka nyumbani mwetu

Tulipiga mbio kuelekea nyumbani

Tulijaribu kadri ya uwezo wetukuuzima lakini ukatushinda

Tulipiga mayowe/ unyende/ kemi za kuitisha msaada

Majirani waliwasili haraka kwa ndoo za maji na matawi ya miti

Miale ya moto ilitafuna nyumba yetu bila huruma

Wanakijiji waliogopa na kukaa kando

Mzee wa kijiji akapigia wazimz moto simu

Wazima moto walikuja upesi na kuuzima moto

Hakuna kiyu kilichobakia

Wazazi wakapigiwa simu

Walipandwa na mori walipowasili kwa kutofuata maagizo

Tulipewa chumba kimoja kwa jirani

Bwana chifu aliongoza mchango wa harambee kuchangisha fedha za kujenga upya nyumba yetu

## SAFARI

Kutembelea mbuga la wanyama

Maandalizi

Kungoa nanga

Njiani waliona nini

Kuwasili

Kupokelewa na kupewa maagizo

Kuwaona wanyama na kupewa maelezo

Kula kishuka

Kujivinjari: kuogelea, kupigwa picha pamoja na wanyama

Kurudi nyumbani

Kuwasili nyumbani na kusimulia jamaa matukio ya siku

Mapambo

Kuamka asubuhi na mapema/ alfajiri mbichi

Kujitayarisha na kiamsha kinywa

Kuwasili shuleni

Kwenda gwarideni/ hotuba ya mwalimu mkuu

Kuwasili kwa basi la kijani kibichi

Kuabiri, dua na kung'oa nanga

Waliona mito, milima, miti, mimea, wanyama, mabonden nyuni, majumba na maziwa

Kuwasili mwendo wa saa nne asubuhi

Tulipokelewa kwa mikono miwili na kupewa maagizo na inspekta kizito

Alikuwa na sauti nyororo

Kutembezwa na kupewa maelezo kuhusu wanyama tofauti

Mimuliko ya kimera ilionekana tulipokuwa tukiwapiga hayawani picha

Kulikaa kitako kando yam to molo kula kishuka kitamu ja uki

Manyani walituvamia na kuubeba mkungu wa ndizi

Mwalimu alitupa jiwe wakatupa maembe

Tuliyaokota, kuyaosha na kuyala

Tulipiga mbizi katika mto Molo

Manyani walizibeba nguo zetu

Tulijilaza kando yam to uchi wa mnyama

Tulivalia sare na kupigwa picha

Malimu alimshukuru mwelekezi wetu

Kuanza safari ya kurudi nyumbani

Kuwasili usiku- giza totoro lilitanda kote

Kukoga, kula chajio na kuwasimulia wavyele matukio ya siku hiyo

Sitaisahau siku hiyo kamwe maishani

MUHULA WA PILI

INSHA

SHEREHE NILIYOHUDHURIA

Kuamka alfajiri na kujitayarisha

- Kuoga na kupiga mswaki
- Kuvalia mavazi nadhifu kama vile kanzu, suti au kizibau

Kunywa staftahi na kuiaga jamaa

- Staftahi kuandaliwa mezani- chai, kahawa tamu kama halua
- Kupewa mawaidha na wazazi-namna ya kuishi na watu –heshima

Kupitia kwa sahibu kumuita

- Kuwasili
- Kupata amejiandaa

Kuelekea kanisani/ msikitini

- Safari- uliabiri gari la aina gani
- Safari ilianza saa ngapi
- Uliketi wapi
- Wingi wa watu/ umati/ halaiki

Kufanyika kwa ibada

- Injili
- Nyimbo kuimbwa
- Sadaka kutolewa

Kuelekea kwenye bustani kujistarehesha

- Kupiga gumzo
- Kupigwa picha
- Kuwaendesha farasi

Kuingia katika ukumbi wa sinema

- Kulipa kiingilio
- Wingi wa watu ndani
- Burudani ya sinema

Kuelekea nyumbani

- Msongamano wa watu na magari
- Kuagana na rafiki
- Kuwasili nyumbani
- Kuwaambia wazazi sherehe ilivyokuwa

Kula na kuenda kulala

- Vyakula vitamu
- Usingizi wa pono

**Hisia za faraja**

Niliingiwa na furaha na buraha

Nilikuwa na furaha ghaya

Niliogelea kwenye bahari ya furaha

Nilifurahi upeo wa furaha yangu

Nilikuwa na faraja mithili ya kibogoyo aliyepata meno, tasa aliyepata motto

**Methali**

Polepole ndio mwendo

Mwenye macho haambiwi tazama

Haraka haraka haina Baraka

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

**Tashbihi**

Ng'ara kama mbalamwezi

Maridadi kama mbega

Ringa kama tausi

Konda kama ng'onda

**Muundo wa sentensi**

Rafiki yangu alikuwa amengara kama mbalamwezi

Nilijitayarisha polepole kwani nlijua kuwa polepole ndio mwendo

Tulipokuwa tukienda kanisani niliona mlolongo wa magari

Nilipoingia katika ukumbi wa sinema niliingiwa na furaha ghaya mithili ya tasa aliyepata pacha

Watu walifurahia sana mithili ya kibogoyo aliyepata menowakati wa mlo

## NDOTO YA AJABU

Kula chajio na kwenda kulala

- Maandalizi ya chakula jioni
- Kulala

Kutekwa nyara pamoja na baba yako

- Kuchukuliwa kwa nguvu
- Kupelekwa kwa meli
- Kukutana na mfalme katili
- Kufanyishwa kazi nzito bila malipo

Kupanga kutoroka

- Kuwatazama ndege wanavyoruka
- Baba kupendekeza wazo la kuruka kama ndege
- Kutengeneza mbawa kutumia nta

Kuanza safari ya kutoroka

- Kuchukua mbawa
- Kuzifunga milini yetu
- Kujaribu kuruka na kufaulu
- Baba kunipa mawaidha nisiruke njuu karibu na jua

Kutotii mawaidha ya baba

- Kupaa hewani
- Kuwakaribia ndege wakubwa
- Kupuuza mawaidha ya baba

- Kuruka juu sana
- Nta kuchomwa na jua
- Mbawa kuharibika
- Kuanguka na kutumbukia baharini
- Kuamka na kushtuka kumbe ni ndoto tu

**Hisia za woga**

- Kijasho chembamba kilinitoka
- Nilitetemeka kama unyasi nyikani
- Nywele zilinisimama timtim
- Viguu vilishindwa kunibeba
- Nilitetemeka kama mbwa mbele ya chatu
- Moyo ulinishuka
- Nilijishika tama

**Methali**

- Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
- Majuto ni mjukuu
- Kilio si dawa
- Maji yakimwagika hayazoleki
- Atangaye sana na jua hujua

**Tanakali za sauti**

- Zama zii

- Rowa rovu rovu
- Moyo kudunda du du du
- Anguka majini chubwi
- Lia kwi kwi kwi
- Vunjika keche
- Dondoka machozi ndo ndo ndo

**Muundo wa sentensi**

Nilianguka baharini chubwi

Sikufuata maagizo ya baba yangu kwani sikujua na kuelewa kuwa asiyesikia la mkuu huvujika guu

Jua lilipochoma nta nilijawa na huzunina nywele zikasimama timtim

Mbawa zilipoharibika nilianza kulia bila kujua kuwa wahenga hawakukosea waliposema kuwa kilio si dawa

Nilipoaga dunia nilizama zi huko baharini

## UMUHIMU WA MAJI

Insha hii inafaa kufuata mtindo huu

Aya ya kwanza hutangulizwa kwa kuelezea maji ni nini na kuelezea zaidi kuhusu maji

Kazi hii hupangwa kwa aya

Kila aya huwa na umuhimu Fulani

Ukitamatisha lkazima aya ya mwisho ihimize sana kuhusu kuyatunza maji na kuyatumia ipasavyo kwasababu ina matumizi sufufu

**Vidokezo**

Maji ni nini?

Maji ni asili ya uhai

Hutumiwa kwa upishi wa vyakula

Hutumiwa kwa usafi wa mwili, mazingira na mavazi

Huzima moto unapoteketeza vitu

Ni makao ya samaki na wanyama wengine

Hutumika katika michezo kv. Kuogelea

Hutumika kwa usafiri

Huzungusha mashine na mitambo ili kutoa nguvu za umeme

Kupoza injini zinapokuwa moto

**Msamiati**

Matumizi kochokocho

Matumizi sufufu

Nishati au nguvu za umeme

Maradhi tumbitumbi

Kustawi na kunawiri

Huimarisha siha

Hamamu na madibwi

Kwenda jongomeo

Mizigo mizito kama nanga

Mchafu mithili ya fuko

Shehena za mizigo

**Vyombo vya usafiri majini**

- Motoboti
- Ngalawa
- Merikebu
- Mashua

**Muundo wa sentensi**

Maji yana matumizi kochokocho kwa binadamu

Maji huzuia maradhi tumbitumbi yanayoweza kuwasafirisha watu hadi jongomeo

Maji huzungusha mitambo na mashine ili kutoa nishati

Maji ya bahari hutumika kusafirisha mizigo mizito mizito kama nanga

Hatuna cha msalie mtume wala nabii ila kuyatumia vizuri

Maji hutumiwa kwa mapishi ya vyakulaambavyo huimarisha siha ya binadamu

Maji hutumiwa kunyunyizia mimea ili kustawi na kunawiri

## NYUMBA YETU

**Vidokezo**

Maana ya nyumba

Aina za nyumba

- Msonge
- Mawe
- Ya udongo
- Ghorofa

Umbo la nyumba yetu

Nyumba inapatikana wapi

Sehemu za nyumba yetu

**Sebuleni: kuna vifaa hivi**

Makochi

Runinga

Zulia

Meza

Kabati

Mapazia

Rafu

Redio

Jokofu

Kinanda

**Jikoni: kuna vifaa hivi**

Vyungu

Birika

Seredani

Kinu na mchi

Bilauri

Sufuria

Vikombe

Sahani

Sinia

**Nyumba ya malazi kuna vifaa hivi**

Vitanda

Blanketi

Magodoro

Mto

Shubaka

Sanduku

Foronya

**Bafuni/ hamamuni**

Sabuni

Taulo

Dodoki

**Msalani**

Karatasi shashi

**Mazingira nje ya nyumba**

- Bustani la maua
- Maegesho
- Kidibwi cha kuogelea
- Miti yenye kivuli

**Tashbihi**

- Ngara kama mbalamwezi
- Nyeupe kama theluji
- Metameta kama nyota angani
- Tamu kama halua
- Maridadi kama mbega

**Misemo**

- Piga mswaki
- Shtaki njaa
- Andika meza
- Piga koga
- Piga mbizi

**Muundo wa sentensi**

Ndani ya jokofu mna sharubati

Mama hutayarishia vyakula jikoni na huwa ni vitamu kama halua

Chakula kitamu kiliandikwa mezani

Dirishani pamefunikwa na mapazia

Nyumba yetu imengara kama mbalamwezi

Sebuleni humetameta kama nyota angani

Nyumba yetu ina kuta za mawe

## AJALI BARABARANI

Ajali ni tukio lenye madhara linalotokea ghafla

Husababisha maafa na majeraha

Mwanafunzi anahitajika kusimulia kisa kinachohusisha magari, baiskeri au pikipiki

Mwanafunzi azingatie:

- Ulikuwa wakati gani ajali ilipotokea
- Alikuwa akielekea wapi
- Ajali yenyewe ilihusisha nini
- Ni nini kilichofuatia baada ya ajali hiyo:
    - hisia za wahusika
    - Kuagiza msaada

**Msamiati**

Kuamka jogoo la kwanza

Demka au rauka majogoo

Piga mswaki

Koga hamamuni kwa dodoki

Kujikwatua kwatu/ kujipamba pambe pambe

Valia libasi zilizongaa kama mbalamwezi

Gari kutiwa moto na dereva/ mshika usukani

Kungoa nanga

Kaa karibu na dirisha kujionea mandhari yaliyovutia

Kujifunga mkanda wa usalama

Piga soga/ gumzo/ porojo

Mwendo wa kasi kama duma/ risasi

Gurafu

Matuta

Yumbayumba

Shindwa kudhibiti gari

Gongana dafrau/ ana kwa ana

Bingirika bingiri bingiri

Vigae vigae

Damu kutiririka tiriri

Machozi yalinipukurika puku puku

Biwi la simanzi lilitanda kote

Kuwanusuru manusura

Kulilia uhai wao

Kupelekwa thieta

Kufungwa plasta

Wafu kupelekwa mochari

Maksa huo utasalia katika kumbukumbu zangu

**Methali**

- Haraka haraka haina Baraka
- Mwenda pole hajikwai
- Kawia ufike
- Pole pole ndio mwendo
- Ajali haina kinga
- Ajali haijali

## CHAKULA NIKIPENDACHO

Chakula ni kitu chochotekinacholiwa na hupa mwili nguvu

**Aina za vyakula**

- ✓ Matoke
- ✓ Mandondo
- ✓ Ugali
- ✓ Vibanzi
- ✓ Mapochopocho
- ✓ Chapati
- ✓ Kimanda

**Mboga na viungo**

- ✓ Tangawizi
- ✓ Nyanya
- ✓ Dania
- ✓ Karoti
- ✓ Kitunguu
- ✓ Biriganya
- ✓ Sukuma wiki

**Tahakiki ya ulaji**

Mapochopocho yaliandaliwa , si nyama, si pilau

Utamu wa chakula hicho ungemfanya mtu kuramba kiwiko cha mkono

Tulinyofua minofu au nyama

Kusharabu vinywaji

Mshumbi wa wali

**Tashbihi**

- ✓ Tamu kama halua
- ✓ Fura kama hamira
- ✓ Laini kama pamba
- ✓ Tengana kama ardhi na mbingu
- ✓ Gumu kama mango

**Methali**

- ✓ Mchumia juani hulia kivulini
- ✓ Alimaye mtama huvuna kunde
- ✓ Tembe na tembe huwa mkate
- ✓ Mgaagaa na upwa hali wali mkavu
- ✓ Mla kunde hunya kunde

**Vifaa vya kupikia**

- ✓ Mafiga
- ✓ Stovu
- ✓ Sahani
- ✓ Birika
- ✓ Bilauri
- ✓ Jokofu
- ✓ Seredani

**INSHA YA KUMALIZIA**

Insha sampuli hii huhusu kisa futuhi (furaha) au tanzia (huzuni)

Mtahiniwa anahitajika kuhitimisha kisa chake kwa maneno aliyopewa

Mtahiniwa alenge swali la mtahini

**Msamiati**

Insha hizi zitahusu:

- ✓ Harusi- akidi, ndoa, nikahi, pingu ya maisha
- ✓ Siku ya kuzaliwa
- ✓ Siku ya kwanza shuleni
- ✓ Sherehe ya krismasi

**Mada**

- ✓ Siku ya siku
- ✓ Siku ya kufana
- ✓ Siku ya ndovu kumla mwanawe
- ✓ Siku ya kukaa na shoka

**Msamiati**

Kuamka/ kurauka/ kudemka alfajiri/ kabla ya jogoo la kwanza

Kunywa staftahi tamu kama halua kwa tende/ asali ya malkia nyuki

Kuvalia mavazi nadhifu kama ubwende

Kujikwatua kwatukwatu/ kujipamba pambepambe

Valia libasi

Wapambe

Mlibwende/ mrembo/ kipusa/ spoti- kike

Mtanashati/ mfuauji – kiume

Kungoa nanga

Abiri gari –mlolongo/ msafara

Umati/ kaumu/ halaiki ya watu

Kufanyika kwa ibada

Kunengua viunoungedhani mola alisahau kuwatia mifupa

Malaika/ hurulaini wa peponi/ ungedhani mungu alichukua siku ayami(nyingi) kumuumba

Mimuliko ya kamera

Furahi ghaya kufurahi

Furaha sufufu/ mpwitompwito

Furahi kama:

- ✓ Kibogoyo aliyepata meno msimu wa krismasi
- ✓ Mama aliyejifungua salama salmini
- ✓ Mvuvi aliyekinasa kishazi cha samaki

Bahatika kama:

- ✓ Mtende
- ✓ Mwana aliyezaliwa siku ya ijumaa

Vyakula – mapochopocho ya kila nui si pilau, si sima ,si wali, si chapatti nk

Vinywaji sampuli sampuli- sharubati, maji matamu, soda nk

**Msamiati wa huzuni**

- ✓ Juhudi kugonga mwamba

- ✓ Mambo kwenda mvange
- ✓ Kijasho chembamba kilianza kumtoka
- ✓ Tiririkwa na machozi kama ngamia
- ✓ Machozi ya majonzi
- ✓ Vilio vya kite na shake
- ✓ Kamasi ilinitonatona
- ✓ Damu ilitiririka kila mahali

# LUGHA

## MUHULA WA PILI

### SURA YA KWANZA

**Msamiati: saa**

Mwalimu atangulize kwa imla

Kueleza msamiati wa saa

Saa ni chombo au kifaa cha kupimia wakati

Dakika: dakika sitini ni saa moja au nzima

Nukta: nukta sitini ni dakika moja. Nukta pia huitwa sekunde

Robo: ni dakika kumi na tano baada ya saa

Kasoro: hutumiwa kueleza kuwa bado dakika Fulani itimie saa Fulani

Kasorobo: bado robo/ dakika kumi na tano

Nusu: ni gdakika thelathini baada ya saa Fulani au bado dakika thelathini saa Fulani itimie

Marejeleo: kurunzi uk 70-72

**Kusoma na kuandika**

Sauti g, ng, nz na z

Kutangulkiza kwa imla ya maneno yenye sauti G, NG, NZ na Z

Mwalimu asome maneno kasha wanafunzi wafuatilie wakitamka

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia baadhi ya maneno

Tathmini: km uk 87

Mwongozo uk 85-86

Mwalimu aongezee maswali mengine uk 87

Mazoezi ya ziada km uk 79

**SURA YA PILI**

Km uk 90-92

Mwongozo uk 88-89

**UFAHAMU: tumbokarai**

Uchambuzi wa picha

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa kutumia msamiati huo

Tathmini: zoezi uk 89

**Sarufi: vivumishi vya sifa**

Vivumishi vya sifa ni maneno yanayotoa sifa kuhusu jina lolote katika ngeli kuelezajinsi jina hilo lilivyo, linavyofanana ama linavyolingana

Vivumishi hivi huchukua viambishi katika umoja na wingi kwa kutegemea ngeli

Mfano

| | | |
|---|---|---|
| U-ZI | uzi mdogo | nyuzi ndogo |
| I-ZI | nyumba kubwa | nyumba kubwa |
| LI-YA | gari zito | magari mazito |

Mwalimu ahusishe wanafunzi katika kusoma jedwali

Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia vivumishi vya sifa mbalimbali

Tathmini: km uk 92-93

Mwongozo uk 90

Wanafunzi wepesi wapewe kurunzi uk 15

**Msamiati na matumizi ya lugha**

Zana za vita: silaha ambazo zinatumika katika kujihami kv rungu mkuki ngao manati kisu upanga

Nyenzo: vifaa halisi, picha za zana za vita

Wanafunzi wataje zana ambazo wanatumia nyumbani

Uchambuzi wa picha na zana hizo na vifaa halisi vinavyopatikana

Wataje majina na kazi za zana hizo

Awape zoezi la kuchora baadhi ya zana hizo na kuandika majina yao kn ala, ngao, uta, manati, nk

Tathmini: km uk 94

Mwongozo uk 91

Kurunzi uk 90-92

**Kusikiliza na kuongea**

Matamshi ya sauti NG

Katika lugha ya Kiswahili, ukitamka ng bila king'ong'o huleta maana tofauti na ng' yenye king'ong'o

Mfano:

Ng,ombe ngombe

Ng,ongo ngongo

Mwalimu asome maneno haya kishawanafunzi watamke baada ya mwalimu

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia baadhi ya maneno

Km uk 94-95

Mwongozo uk 91-93

Zoezi uk 95

**Kusoma : ufahamu watoto kumi**

Kutanguliza kwa imla ya ng na ng'

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa kutumia msamiati huo

Mwalimu achambue ufahamu

Tathmini: uk 97-98

Mwongozo 93-94

Km uk 96

**SURA YA TATU**

**Sarufi: viwakilishi au vibadala viwakilishi vya**

Hivi ni viambishi vinavyowakilisha nafsi au jina

Vinatajwa badala ya nafsi au badala ya jina

Mfano

| Nafsi | viwakilishi |
|---|---|
| ✓ Mimi | ni |
| ✓ Sisi | tu |
| ✓ Wewe | u |
| ✓ Nyinyi | m |
| ✓ Yeye | a |
| ✓ Wao | wa |

Mwalimu awahusishe wanafunzi katika kulisoma jedwali

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi

Tathmini: km uk 98-99

Mwongozo uk 94-97 Zoezi uk 99

Kkd uk 38

Kurunzi uk 31

**Msamiati na matumizi ya lugha**

Majina ya makundi

Majina ya makundi ni majina ya vitu vilivyowekwa pamoja kv umati watu, bunda la noti

Mwalimu atumie mifano inayoeleweka kv tita la kuni au bunda la pesa

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuisoma mifano ya nomino za makundi

Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia nomino hizo za makundi

Tathmini: km uk 100

Mwongozo 97-98

Kurunzi 147

Kkd 103

**Kusoma na kuandika**

Matamshi ya sauti NJ, NCH na Y

**Mifano**

| | | |
|---|---|---|
| Njaa | Mwananchi | Fuja |
| Njama | Nchi | Ajili |

Mwalimu atangulize kwa imla ya sauti f na v

Mwalimu aisome orodha ya maneno kisha wanafunzi wayatamke baada yake

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia baadhi ya maneno hayo

Tathmini: km uk 100-101

Mwongozo uk 98-100

Mwalimu awasomee wanafunzi sentensi kutokana na mwongozo

Mwalimu aongezee maswali mengine

**Kusikiliza na kuongea**

Kutunga sentensi

Mwalimu atangulize kwa kuwauliza wanafunzi wataje majina yoyote yenye silabi j n ach kama vile jaa, cheti, chozi, jangili

Mwalimu atoe mifano na kutunga sentensi huku wanafunzi wakisikiliza

Wanafunzi waelekezwe kusoma mifano katika vitabu vyao

Tathmini: mwalimu awape wanafunzi maneno watunge

Km uk 101

**Sarufi: majina kutokana na vitenzi**

Wanafunzi watambue vitenzi na majina km

| **Kitenzi** | **jina la kitendo** | **jina la mtendaji** |
|---|---|---|
| Pika | upishi | mpishi |
| Soma | somo | msomaji |
| Lima | kilimo | mkulima |
| Andika | mwandiko | mwandishi |

Mwalimu awaongoze wanafunzi kuisoma mifano kwenye jedwali

Wanafunzi wataje mifano mingine inayoonyesha majina kutokana na vitenzi

Tathmini: zoezi uk wa km 102

Mwongozo uk 101-102

Kkd uk 106

**SURA YA NNE**

UFAHAMU: hadithi isiyo na mwisho

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja

Kuteua wanafunzi ambao watasoma

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa kutumia msamiati huo

Kuwapa wanafunzi fursa ya kusoma kimoyomoyop

Tathmini: km uk 103-104

**Sarufi: vivumishi vya idadi**

Vivumishi vya idadi hutumika kuonyesha jumla ya namba au kiasi cha vitu vilivyohesabiwa au vinavyoorodheshwa au kupimwa

Km

| | | |
|---|---|---|
| KI-VI | kitabu kimoja | vitabu vinne |
| LI-YA | daftari moja | madaftari kumi |

Vivumishi visivyochukua viambishi vya ngeli ni sita , saba, tisa na kumi

Wanafunzi waongozwe kuisoma mifano vitabuni mwao

Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia vivumishi mbalimbali vya idadi

Tathmini: km uk 104-104

Kkd uk 92

**Msamiati na matumizi ya lugha**

Vifaa vya ufundi kv nyundo, parafujo, misumari, randa, bisibisi, msumeno, utepe, timazi, jiriwa, patasi, msasa nk

Uchambuzi wa picha na vifaa halisi vinavyopatikana

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kazi mbalimbali za vifaa vya ufundi

Watunge sentensi kwa kutumia vifaa vya ufundi

Tathmini: km uk 106

Mwongozo uk 105-106

Kurunzi uk 79-81

**Kusoma na kuandika**

Matamshi ya sauti p na b

| **P** | **b** |
|---|---|
| Papa | baba |
| Pata | bata |
| Pipi | bibi |
| Punda | bunda |

Kutanguliza kwa imla ya ch na sh

Mwalimu aisome orodha ya maneno kasha wanafunzi wasome baada ya mwalimu kwa matamshi bora

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia baadhi ya maneno

Tathmini:

Km uk 106

Mwalimu aongeze maswali mengine

**Kusoma**

**Ufahamu: nazi na jiwe**

Uchambuzi wa picha

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja

Kuhusisha wanafunzi katika usomaji

Kuchambua ufahamu na kueleza ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati huo

Wanafunzi wapewe fursa ya kusoma kwa kiada

Tathmini: km uk 109

Km uk 114 mazoezi ya ziada

**SURA YA TANO**

**Sarufi**

**Ngeli ya KI-VI**

Mwalimu atangulize kwa imla katika ngeli ya LI-YA

Ngeli hii ni majina ya kawaida yanayoanza kwa kiambishi KI kwa umoja na huwa VI kwa wingi

Kiatu viatu

Kioo vioo

Majina mengine huanza kwa CH na wingi VY

Chakula vyakula

Wanafunzi wataje mifano mingine katika ngeli hii

Wahusishwe katika kusoma orodha ya mifano na kutunga sentensi

Tathmini: km uk 110-111

Mwongozo uk 110-112

Mwalimu aongezee maswali mengine

**Kusikiliza na kuongea**

**Misemo au nahau**

Misemo ni fungu la maneno linalotumiwa kwa maana iliyofichika kv

| | |
|---|---|
| Kula chumvi nyingi | kuishi miaka mingi |
| Kushika mkia | kuwa wa mwisho |
| Kula mwata | kupata taabu |

Wanafunzi waruhusiwe kuitaja mifano ambayo wanaifahamu

Waelekezwe kuisoma mifano mbalimbali vitabuni ya misemo. Aidha watunge sentensi kwa kuitumia baadhi ya misemo

Tathmini: km uk 111-112

Mwongozo uk 1122

Kkd uk 25

Kurunzi uk 121

**Kusoma na kuandika: matamshi ya M, MU na MW**

Kutanguliza kwa imla ya maneno yenye sauti p na b

| | | |
|---|---|---|
| Mu | m | mw |
| Mufti | mmesafiri | mwizi |
| Muhimu | tulimpa | sitamwona |

Mwalimu asome maneno na sentensi katika vitabu

Wanafunzi wasome wenyewe baada ya mwalimu

Wanafunzi waorodheshe majina hayo madaftarini

Wapewe fursa na kutunga sentensi fupifupi

Tathmini: km uk 113

Mwongozo uk 114

Wanafunzi waandike imla kwa mwongozo wa mwalimu 1-10

**Mtungo: kuandika imla: sauti za dh na th**

Wanafunzi wataje matamshi ya hapo awali kv f na v, awaambie waunde maneno wakitumia silabi hizo

Wataje matamshi mengine kama r na l, s na z, nk

Mwalimu awaagize wanafunzi kutamka maneno yenye sauti dh na th mmoja baada ya mwingine

Tathmini:

Mwalimu awatayarishe wanafunzi wawe makini kunakili madaftarini mwao maneno ya sauti dh na th

Km uk 113

Mwongozo uk 115

**Kusoma : ufahamu nyama nzuri na mbaya(2)**

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusu ufahamu waliosoma sehemu ya kwanza. Wataje matukio yaliyojiri

Waeleze msamiati waliojifunza na kutunga sentensi

Wanafunzi waelekezwe kusoma ufahamu zaidi ya mara moja. Aidha wausome kwa kiada

Kuchambua ufahamu na ujumbe ulioko

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa msamiati

Tathmini: km uk 115-116

Mwongozo uk 116-118

Km uk 114 mazoezi ya ziada

**SURA YA SITA**

**Sarufi: kiambishi ki cha udogo**

Ukitaka kubadili jina katika hali ya udogo unapachika kiambishi ki mwanzo wa jina la ukubwakv

| | |
|---|---|
| Jitu | kijitu |
| Jibwa | kijibwa |
| Buzi | kibuzi |
| Toto | kitoto |

Wanafunzi waelezwe hali tatu za majina na wapewe mifano wastani, ukubwa na udogo

Wahusishwe katika kusoma mifano na sentensi

Wahusishwe kutunga sentensi mbalimbali

Tathmini: km uk 117

Mwongozo uk 119

Kkd uk 42-43

Kurunzi uk 62-63

**Msamiati na matumizi ya lugha**

**Hali ya anga**

Mbingu, nyota, sayari, jua, upepo, mawingu, ukungu, baridi, vimondo, umeme, nk

Vyombo vipima hewa: kipima upepo, kipima mvua, nk

Misimu: kiangazi, kipupwe, mchoo au vuli, kusi, kaskazi na matlai

Mwalimu awatoe wanafunzi nje na kuelezea vitu ambavyo wanaviona

Waeleze vile ambavyo huonekana usiku

Wanafunzi watambue vyombo au vifaa mbalimbali

Aidha mwalimu awahusishe wanafunzi kutambua misimu ainati

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati

Tathmini: km uk 117-118

Mwongozo uk 119-120

**Kusoma: ufahamu: mzee Domo**

Uchambuzi wa picha

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Kuhusisha wanafunzi katika usomaji

Kuchambua ufahamu na kueleza ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati

Tathmini: km uk 121-123

Mwongozo uk 124

**Sarufi: tashbihi(vifananisho)**

Tashbihi ni maneno ya kufananisha au kulinganisha vitu, mambo, watu, hali au maumbile

Kama: mwaminifu kama mchana

Mrefu kama mlingoti

Wanafunzi wapewe fursa ya kutaja mifano ya tashbihi wanayojua

wahusishwe kuisoma mifano vitabuni

aidha watunge sentensi kwa kutumia tashbihi

tathmini: km uk 123-124

mwongozo 124

kurunzi 93-94

mazoezi ya ziada km uk 127

## SURA YA SABA

**Msamiati na matumizi ya lugha: ala za muziki**

Kutaja imla ya s n ash

Ala za muzikzi ni vyombo au vifaa vinavyotumiwa katika kutoa sauti

Kama vile:

- ✓ kayamba
- ✓ Tari
- ✓ Ngoma
- ✓ Gitaa
- ✓ Zeze
- ✓ Marimba
- ✓ Tarumbeta
- ✓ Zumari
- ✓ Kinubi

Wanafunzi watambue majina ya ala na vifaa halisi kama ngoma na tari

Mwalimu aeleze mbinu zinzzotumika kucheza ala mbalimbali kv kutikisa, kupuliza au kupiga

Mwalimu awahusishe wanafunzi kueleza faida za muziki katika jamii

Tathmini: km uk 124-125

Mwongozo uk 68-70

Kurunzi uk 116

**Kusoma na kuandika: shairi**

**Ulegevu ni adui**

Kutanguliza kwa imla ya viishio ua na wa

Shairi ni aina ya wimbo ambao unafuata kanuni au sheria

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kulighani shairi na kutamka maneno kwa ufasaha

Mwalimu aeleze maana ya maneno yafuatayo ya ushairi:

- ✓ Kibwagizo
- ✓ Ubeti
- ✓ Mshororo
- ✓ Mizani

- ✓ Kina/ vina

Bahari ya shairi

Tathmini: mufti uk 125

Mwongozo uk 127-128

Kkd uk 34

**Kusoma : ufahamu**

**Sungura na zabibu**

Uchambuzi wa picha

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja kwa kiada

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa baadhi ya msamiati

Mwalimu auchambue ufahamu

Tathmini: km uk 128-129

Mwongozo uk 132-133

**Kusikiliza na kuongea: kusimuliana hadithi**

Mwalimu aeleze kuwa hadithi pia huitwa ngano

Aelezee mianzi ya hadithi kv:

- ✓ Paukwa pakawa
- ✓ Hapo zamani za kale
- ✓ Hapo jadi na jadudi

Wanafunzi wapewe fursa ya kusimulia hadithi fupifupi zenye mafunzo

Wanafunzi wasome hadithi moja na wajibu maswali darasani

Tathmini: kurunzi uk 33-34

Km uk 131

## SURA YA NANE

**Kusoma na kuandika: ufahamu:**

**Bahari inawaka moto**

Kutanguliza kwa imla y ach n ash

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja kwa kiada

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati

Mwalimu achambue ufahamu

Tathmini: km uk 132-133

Mwongozo uk 135

**Sarufi**

**Vikanushi vya ngeli**

Kutanguliza kwa imla ya maneno ya ngeli ya I-ZI

Mwalimu aeleze kukanusha ni kukataa

Aelezee kuwa ukiambatanisha kiambishi chochote cha ngeli na HA utapata kikanushi kamili cha kila ngeli

Awape mifano ya vikanushi vya ngeli

Awahusishe katika kutunga sentensi

Tathmini: km uk 135-136

Mwongozo uk 137-138

Kkd uk 27

**Msamiati na matumizi ya lugha kua na kuwa**

Kutanguliza kwa imla ya maneno yenye sauti sh na z

Kua: hutumika unapotaja umri/ miaka/ kunenepa

Kuwa: hutumikakuonyesha kufanyika kwa kitendo au kupatikana kwa mtu au kitu

Mwalimu atunge sentensi kuelezea vitenzi hivi

Awahusishe wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali kwa vitenzi hivi

Tathmini: km uk 130-131

Mwongozo uk 132-133

**Matumizi ya lugha:Mnyambuliko wa vitenzi**

Mnyambuliko ni mabadiliko mbalimbali ya vitenzi ili kuleta maana n nia tofauti

**Mifano**

| | | |
|---|---|---|
| Kutenda | kutendea | kutendewa |
| Kupiga | kipigia | kupigiwa |
| Kuandika | kuandikia | kuandikiwa |

Mwalimu awaeleze wanafunzi jinsi ya kunyambua vitenzi katika kauli mbalimbali

Wanafunzi wahusishwe katika kulisoma jedwali na baadaye kutunga sentensi mbalimbali

Tathmini: km uk 135-136

Mwongozo uk 138-139

Kkd uk 64-65

Kurunzi uk 118

**Kusoma na kuandika**

**Shairi: kesho wewe**

Kutanguliza kwa imla ya sauti g na ng

Wanafunziwaelekezwe jinsi ya kulighani shairi na kutamka maneno kwa ufasaha

Mwalimu ajadiliane na wanafunzi maneno mapya na jinsi yalivyotumika katika shairi

Awaulize maswali ya beti, mishororo, vina, kibwagizo na mizani

Tathmini: km uk 136

Mwongozo uk 140

**SURA YA TISA**

**Kusoma ufahamu:** Maboga ya nyanya(sehemu ya pili)

Uchambuzi wa picha

Kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Kuhusisha wanafunzi katika usomaji

Kueleza ujumbe ulioko na kuchambua ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kutumia msamiati huo

Tathmini: km uk 139-141

Mwongozo uk 142

**Sarufi: uakifishaji**

Mwalimu atangulize kwa imla ya sauti b na p

Wanafunzi waelekezwe jinsi ya kutumia alama za uakifishaji na kuzitambua alama hizo kama vile:

- ✓ Kikomo
- ✓ Kipumuo

- ✓ Kiulizi
- ✓ Hisi
- ✓ Mtajo

Wanafunzi waelekezwe kwa kusoma maelezo yaliyo kwenye vitabu

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi kutumia alama za uakifishaji

Tathmini: km uk 141-142

Mwongozo uk 143

Kkd uk 23-24

**Matumizi ya lugha**

**Michezo**

Mwalimu atangulize kwa imla ya sauti z na s

Mwalimu awaeleze wanafunzi kutambua michezo Mbalimbali kama vile: kandanda

- ✓ Kwata
- ✓ Sarakasi
- ✓ Mpira wa magongo
- ✓ Mpira wa pete
- ✓ Mpira wa vikapu

Wanafunzi wajulishwe kuhusu michezo hii..

Mwalimu atumie picha na vifaa halisi vinavyopatikana

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia majina ya michezo

Tathmini: km uk 142

Mwongozo uk 144

Kurunzi uk 104

**Kusoma na kuandika**

**Shairi: wema hatunao**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya sauti dh na th

Wanafunzi waelekezwe kughani shairi kwa mahadhi

Mwalimu ajadili maneno magumu yaliyotumiwa

Wanafunzi wataje kuhusu beti, mishororo, kibwagizo, vina na mizani

Tathmini: km uk 143-144

Mwongozo uk 145-146

Kurunzi uk 143-144

**Mtungo: maneno tatanishi(vitate)**

Kutanguliza kwa imla ya sauti za viishio ua na wa

Mwalimu ayatamke maneno nao wanafunzi watamke baada ya mwalimu

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi kwa kutumia maneno tatanishi

**Mfano:**

Kura zilipigwa baada ya kula chakula

Kuku anachoka ili apate chakula

Motto amekua na kuwa m,kubwa

Tathmini: km uk 144

Mwongozo uk 146

Kkd uk 5-6

Mazoezi ya ziada km uk 146-147

## MUHULA WA TATU

### SURA YA KWANZA

**Ufahamu: mahafali**

Kutanguliza kwa imla ya maneno ya vitate

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma zaidi ya mara moja na kwa ziada na kwa kiada

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati

Tathmini: km uk 149

Mwongozo uk 148-149

**Sarufi: ngeli ya U-ZI(marudio)**

Kutanguliza kwa imla ya maneno katika ngeli ya I-ZI

**MFANO:**

| **U-NY** | | **U-ND** | | **U-MB** | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uzi | nyuzi | Ulimi | ndimi | ubawa | mbawa |
| Unywele | nywele | Udevu | ndevu | ubavu | mbavu |
| Unyasi | nyasi | | | | |

| **U** | | **W-NY** | | |
|---|---|---|---|---|
| Ufunguo | funguo | wimbo | | nyimbo |
| ubeti | beti | wavu | nyavu | |
| Ufagio | fagio | waya | nyaya | |

Wanafunzi waelekezwe kubainisha viambishi na viwakilishi katika ngeli hii kwa umoja na wingi

Wanafunzi waelekezwe kuisoma mifano ya maneno na sentensi

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga sentensi

Tathmini: km uk 151-152

Mwongozo uk 149

**Matumizi ya lugha**

Majina kutokana na vitenzi(marudio)

Kutanguliza kwa imla ya maneno yenye sauti f na v

Mwalimu atoe mifano ya vitenzi na nomini

| **Kitenzi** | **nomino** |
|---|---|
| ✓ Hukumu | hakimu |
| ✓ Ongoza | kiongozi |
| ✓ Kufa | mfu |
| ✓ Iba | mwizi |
| ✓ Tunga | mtunzi |
| ✓ Vua | mvuvi |

Wanafunzi waelekezwe kusooma mifano mbalimbali na kutunga sentensi

Tathmini: km uk 152

Mwongozo uk 149-150

Kkd uk 106

Kurunzi uk 139-140

**Kusoma na kuandika**

**Shairi: mama amenikimbia**

Wanafunzi waelekezwe jinsi ya kulighana shairi na kutamka maneno kwa ufasaha

Mwalimu aeleze msamiati uliotumika

Ajadiliane na wanafunzi kuhusu beti, mishororo, vina, kibwagizo na mizani

Kutaja bahari ya mashairi kv thathlitha, tarbia, tathnia

Tathmini: km uk 152-153

Mwongozo uk 150-152

**Kusikiliza na kuongea**

Sentensi zenye majina, vivumishi, vielezi na vitenzi

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti s na z

Mwalimu aeleze maana ya maneno haya: majina, vivumishi, vitenzi na vielezi

| **Majina** | **vivumishi** | **vitenzi** | **vielezi** |
|---|---|---|---|
| Kuku | mdogo | amekimbia | sana |
| Maziwa | matamu | yananywewa | zaidi |
| Kisu | butu | kinakata | polepole |

Wanafunzi wahusishwe katika kutaja mifano na sentensi mbalimbali kwa kufuata mtindo ufaao

Tathmini: km uk 153-154

Mwongozo uk 152-153

Km uk i54 mazoezi ya ziada

## SURA YA PILI

**Ufahamu: bahati ya ziwakulu**

Kutanguliza kwa imla ya sauti ya p na b

Kuhusisha wanafunzi kusoma zaidi ya mara moja na kwa makini zaidi

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati huo

Mwalimu achambue ufahamu

Tathmini: km uk 156-158

Mwongozo uk 154

**Sarufi: miundo ya vitenzi**

Kutanguliza kwa imla yenye sauti ya r na l

Mwalimu awaeleze wanafunzi jinsi ya kuunda vitenzi kutokana na majina na kuunda vitenzi kutokana na majina ya watendaji

Mifano

| **Majina** | **vitenzi** |
|---|---|
| Mchezo | cheza |
| Wimbo | imba |
| Masomo | soma |
| Ulinzi | linda |
| **Watendaji** | **vitenzi** |
| Mchezaji | cheza |
| Wagomaji | goma |
| Msomaji | soma |
| Mlinzi | linda |

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga vitenzi na sentensi mbalimbali

Tathmini: km uk 158

Mwongozo uk 155-156

**Matumizi ya lugha**

**Majina ya makundi**

Majina ya makundi ni majina ya vitu vilivyowekwa pamoja kama:

- ✓ Thurea ya nyota
- ✓ Mlolongo wa magari

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti dh na th

Mwalimu atumie mifano inayoeleweka kama:

- ✓ Umati wa watu
- ✓ Tita la kuni

- ✓ Bunda la noti

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuisoma mifano ya nomino za makundi

Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia baadhi ya nomino za makundi

Tathmini: km uk 158-159

Mwongozo uk 156

Kurunzi uk 147

**Kusoma**

**Shairi: mtenda hutendwa**

Kutanguliza kwa maneno ya imla yenye sauti ny na y

Wanafunzi waelekezwe kughani shairi kwa mahadhi

Mwalimu ajadili maneno magumu yaliyotumiwa

Wanafunzi waongozwe kuhusu beti, mishororo, kibwagizo, vina ,mizani

Tathmini: km uk 159-160

Mwongozo 158-159

**Kusikiliza na kuongea**

**Maswala ya kimazingira**

Kutanguliza kwa maneno ya imla yenye sauti p na b

Mazingira ni hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anayoishi au maisha yake

Mwalimu awapeleke wanafunzi nje ili watazame mandhari

Wanafunzi wataje faida za kudumisha usafi wa mwili na mazingira

Mwalimu awagawe kwenye makundi ili awape mijadala

Tathmini: km uk 161-162

Mwongozo uk 160

Mazoezi ya ziada km uk 161

## SURA YA TATU

### KUSOMA UFAHAMU

**Mke wa mvuvi (sehemu ya pili)**

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi katika kusoma zaidi ya mara moja

Mwalimu achambue ufahamu na kueleza ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kutumia baadhi ya msamiati

Tathmini: km uk 165

Mwongozo uk 162

Kkd uk 42

Kurunzi uk 62

**Sarufi: kiambishi ki –cha udogo (marudio)**

Ukitaka kubadili jina katika hali ya udogo unapachika kiambishi ki mwanzo wa jina la ukubwa

Mwalimu atangulize kwa maneno yenye sauti gh na h

**Mifano**

- Ukubwa udogo
- Jibwa kijibwa
- Jitu kijitu
- Jisu kijisu

- Gombe kigombe
- Buzi kibuzi
- Jumba kijumba

Wanafunzi waelezwe hali tatu za majina na wapewe mifano wastani, ukubwa na udogo

Wahusishwe katika kutunga sentensi mbalimbali

Tathmini: km uk 165

Mwongozo uk 162

Kkd uk 42

Kurunzi uk 62

**Msamiati na matumizi ya lugha**

**Ukoo(marudio**)

Mwalimu atangulize kwaa maneno ya imla yenye sauti b na mb

Mwalimu aeleze majina ya ukoo kama shangazi halati binamu kilebwe, mjukuu, mkazamwana, wifi, shemeji, kining'ina nk

Wanafunzi wapewe fursa ya kutaja na kuelezea baadhi ya majina ya ukoo wanayoyafahamu

Mwalimu aeleze baadhi ya msamiati kv kilebwekeza, mkazamwana, mpwa, mkoi,nk

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi mbalimbali kwa kutumia baadhi ya msamiati wa ukoo

Tathmini: km uk 166

Mwongozo uk i64

Kurunzi uk 29

Km uk 57

**Kusoma: ng'ombe na fisi**

Uchambuzi wa picha

Kutanguliza kwa maneno ya imla yenye sauti r na l

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Mwalimu achambue ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi kwa baadhi ya msamiati

Tathmini:

Kkd uk 10

Mwongozo uk 9-11

**Kusikiliza na kuongea**

**Vitendawili**

Vitendawili ni maneno yanayoficha maana ya kitu ili kkisijulikane kwa urahisi

Mwalimu atangulize kwa kuwapa wanafunzi imla ya methali fupifupi

Wanafunzi wategeane vitendawili kwenye vitabu vyao vya kusoma

Tathmini: kurunzi uk 65-67

Ziada km uk 167

## SURA YA NNE

**Ufahamu: barua**

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti CH, J na SH

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Kuchambua ufahamu na kuelezea ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutunga sentensi kwa kutumia baadhi ya msamiati

Tathmini: km uk 169-170

Mwongozo uk 171-172

**Sarufi: kirejeshi amba(marudio)**

Mwalimu aeleze kuwa kirejeshi amba huchukua viambishi vya ngeli

Wanafunzi wahusishwe katika kusoma orodha ya mifano kwenye vitabu

Aidha waandike sentensi ambazo zina –amba na nyingine ambazo hazina

Wanafunzi wahusishwe kutunga sentensi kwa kutumia amba

Tathmini: km uk 171

Mwongozo uk 167-168

**Msamiati: mazoezi ya mseto**

Mwalimu atangulize kwa imla ya vitate

Wanafunzi wahusishwe na kuukizwa maswali ya aina mbalimbali

Wahimizwe kusoma maswali kwa makini na maagizo waliyopewa

Tathmini: km uk 172

Mwongozo uk169

**Kusoma na kuandika**

b

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti ch n ash

Mwalimu awafunze wanafunzi kuhusu uakifishaji bora. Awape sentensi na wazisome wakizingatia vituo, vikomo, hisi na viulizi

Wanafunzi wapewe fursa ya kusoma sentensi hizo kwa sauti akisikiliza matamshi yao

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

Tathmini: km uk 172-173

Mwongozo uk 170

**Kusikiliza na kuongea**

**Hadithi**

Mianzo ya hadithi hadithi njoo….

Mwalimu asimulie hadithi fupi

Wanafunzi wapewe fursa ya kusimulia hadithi fupifupi zenye mafunzo

Darasa lote lihusishwe katika kusoma hadithi moja na kujibu maswali

Tathmini: kkd uk 90-91

Mazoezi ya ziada km uk 173-174

## SURA YA TANO

**Kusoma : ufahamu**

**Umleavyo ndivyo akuavyo**

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Kueleza ujumbe ulioko na kuchambua ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 175-176

Mwongozo uk171

**Sarufi: ngeli ya U-U**

Kundi hili ni la majina ya hali, sifa na vitu vishikamano ambavyo havibadiliki katika

umoja na wingi

Kama vile

- Muda
- Ubaya
- Uhodari
- Uzima
- Moshi
- Uhai
- Uhuru
- Wizi

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla ngeli ya U-ZI

Wanafunzi wahusishwe katika kusoma orodha ya majina katika ngeli ya U-U na miundo ya sentensi

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga sentensi

Tathmini: km uk 177-178

Mwongozo uk 172-174

**Matumizi ya lugha**

**Mazingira yetu: mjadala**

Mjadala: mazungumzo juu ya jambo maalum yanayofanywa kwa kutolea hoja kihusu jambo hilo: mashindano ya maneno; mdahalo

Mwalimu awaulize wanafunzi wajadiliane na kueleza kuhusu picha kwenye vitabu vya wanafunzi

Wanafunzi watoe hojambalimbali na wawe na uhuru wa kutoa maoni yao

Tathmini: km uk 178-179

Mwongozo uk 174-175

**Kusoma na kuandika**

**Hadithi: motto iendee haki yako**

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti f na v

Mwalimu aweze kueleza kuhusu mianzo ya hadithi

Wanafunzi wahusishwe katika kusoma hadithi na kujibu maswali ya hadithi

Tathmini: km uk 180-181

Mwongozo uk 175-176

**Mtungo: kujaza mapengo**

Mwalimu aanze kwa kuwapa wanafunzi imla ya vitate

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuhusu a unganifu katika ngeli zote kwa umoja na wingi

| | | | |
|---|---|---|---|
| A-WA | KI-VI | I-ZI | U-ZI |
| Motto wa | kitanda cha | karatasi ya | ukuta wa |
| Watoto wa | vitanda vya | karatasi za | kuta za |

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga sentensi

Tathmini: km uk 181

Mwongozo uk 176-177

Zoezi la ziada km uk 181-182

## SURA YA SITA

**Kusoma: ufahamu**

**Sungura kizimbani (sehemu ya kwanza)**

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Kueleza ujumbe ulioko na kuchambua ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 183-184

Mwongozo 177-179

**Sarufi: kukanusha nyakati**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti b na mb

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusu vikanushi kuhusu nyakati mbalimbali

Kama:

- Me hukanushwa na kuwa ja
- Li hukanushwa na kuwa ku
- Ta hukanushwa na kuwa ta

Wanafunzi watunge sentensi fupi wakitumia nyakati zozote na kasha kuzikanusha

Tathmini: km uk 185

Mwongozo uk 179-180

**Msamiati na matumizi ya lugha**

Mwalimu atangulize kwa imla ya vitate

Mwalimu awakumbushe wanafunzi matumizi ya semi au nahau

Wanafunzi wataje misemo ambayo wanaifahamu vizuri. Aidha watunge sentensi kwa kutumia misemo mbalimbali

Tathmini: km uk 185-186

Mwongozo uk 180

**Kusoma**

**Hadithi**

Mwalimu atangulize kwa kuwapa wanafunzi imla ya vitate

Mwalimu aweze kueleza kuhusu mianzo ya hadithi

Wanafunzi wahusishwe katika kusoma hadithi na kujibu maswali husika

Mwalimu aelezee msamiati uliotumika katika hadithi

Tathmini: kurunzi uk 42-44

**Mtungo**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti sh n ach

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusu maendelezo ya maneno na uakifishaji

Ataje baadhi ya maneno ambayo huwakanganya wanafunzi katika maendelezo na matamshi

Tathmini: km uk 193

Mwongozo uk 189-190

Mazoezi ya ziada km uk 194

## SURA YA SABA

**Kusoma :ufahamu**

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja

Mwalimu acahmbue ufahamu na kueleza ujumbe ulioko

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 189-191

Mwongozo 183

**Sarufi**

**Kivumishi cha pekee-ote**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti p na b

Mwalimu aelezee matumizi ya –ote katika ngeli tofauti

| A-WA | I-ZI | U-ZI | LI-YA |
|---|---|---|---|
| Wanyama wote | nguo zote | uzi wote | gari lote |
| | | nyuzi zote | magari yote |

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga sentensi kwa kutumia –ote

Wanafunzi wahisishwe katika kuisoma mifano yote

Tathmini: km uk 192

Mwongozo uk 185-187

**Matumizi ya lugha**

**Mafumbo na vitendawili**

Mwalimu apeane imla ya maneno yenye sauti tata

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu kutegua vitendawili na kufumbua mafumbo

Wanafunzi wahusishwe katika kutegua vitendawili na kufumbua mafumbo

Tathmini: km uk 192

Mwongozo uk 187-188

**Kusoma: hadithi**

**Siku ya mauti**

Mwalimu awape wanafunzi maneno ya imla yenye sauti ng na ng'

Wanafunzi wakubushwe kuhusu usomaji kv. Kutumia vidole, kuweka vitabu mahali pema dawatini

Kusoma kwa kiada bila sauti yoyote

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma hadithi na hatimaye wayajibu maswali

Tathmini: kurunzi uk 75

**Kuandika: mtungo**

Mwalimu awape wanafunzi imla ya maneno yenye sauti y na ch

Wanafunzi waelezwe kuhusu mtiririko wa mtungo barabara

Waelezwe kutumia lugha ipasavyo

Wahimizwe kutaja ngeli walizofunzwa na kujaza mapengo kwa majibu yafaayo zaidi

Tathmini: km uk 200

Mwongozo uk 203

Mazoezi ya ziada km uk 201

**SURA YA NANE**

**Kusoma: ufahamu**

**Inda za mbwa**

Kutanguliza kwa imla za vitate

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kina zaidi

Mwalimu auchambue ufahamu na kueleza ujumbe ulioko katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 196-198

Mwongozo 190-191

**Sarufi**

**Umoja na wingi wa sentensi**

Mwalimu atangulize kwa kwa kupeana imla ya sentensi kwa umoja na wingi

Wanafunzi wahusishwe kutaja nomino kwa umoja na wingi katika ngeli mbalimbali

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

Wanafunzi wakumbushwe kuhusu vimilikishi, viwakilishi na viambishi

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi kwa umoja na wingi

Tathmini: km uk 198-199

Mwongozo uk 193

**Matumizi ya lugha**

**Afya na usafi**

Afya ni hali nzuri ya mwili bila maradhi yoyote ilhali usafi ni hali ya kutokuwa na uchafu

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti r na l

Wanafunzi wahusishwe katika kujadili mambo muhimu kuhusu afya na usafi maishani

Vilevile mwalimu awafunze kuimba wimbo wa afya

Tathmini: km uk 198-199

Mwongozo uk 193-194

**Kusoma**

**Shairi: panya**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti s na z

Wanafunzi waongozwe kulighani shairi kwa ufasaha

Mwalimu aelezee kuhusu maneno magumu

Mwalimu awahusishe wanafunzi kuelezea maana ya vina, ubeti, mishororo, mizani na kibwagizo

Tathmini: km uk 186-187

Mwongozo uk 181-182

**Mtungo**

**Mjadala**

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

Maisha ya mashambani ni bora kuliko ya mjini

Mwalimu awaeleze kuhusu kuuendeleza mjadala

Mwalimu awagawanye katika vikundi

Ahimize kuwa lugha nzuri itumiwe

Wanafunzi wachangie kwa kutoa hoja ainati

Aidha wanafunzi wazingatie fani mbalimbali kv. Methali, tashbihi, istiara na nahau

Tathmini: km uk 183

Mwongozo uk 182

Mazoezi ya ziada km 187-188

## SURA YA TISA

**Kusoma: ufahamu**

**Zilizala**

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Mwalimu auchambue ufahamu na kueleza ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 202-203

Mwongozo 195-197

**Sarufi**

**Matumizi ya amba**

Mwalimu atangulize kwa imla ya maneno yenye sauti f na v

Wanafunzi wakumbushwe kuhusu matumizi ya amba

Km

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

Wimbo ambao utaimbwa nyimbo ambazo zitaibwa

Koti ambalo limevaliwa makoti ambayo yamevaliwa

Uga ambao utachezewa nyuga ambazo zitachezewa

Punda ambaye atavuta rukwama punda ambao watavuta rukwama

Wanafunzi wapewe fursa ya kutunga sentensi katika ngeli zozote walizosoma kwa amba

Tathmini: km uk 203-204

Mwongozo uk 197-198

Kurunzi uk 53

**Matumizi ya lugha**

**Methali na tashbihi**

Wanafunzi wataje mifano mbalimbali ya methali na tashbihi

Mwalimu awahusishe wanafunzi katika kuelezea baadhi ya methali na tashbihi

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia methali na tashbihi ambazo wanafahamu barabara

Tathmini: km uk 204

Mwongozo uk 198-199

Kkd uk 78

**Kusoma**

**Shairi: dunia hasama**

Mwalimu atangulize kwa maneno ya imla yenye sauti d na nd

Wanafunzi waongozwe kulighani shairi kwa ufasaha

Mwalimu alichambue shairi na aelezee kuhusu msamiati uliotumika

Mwalimu awahusishe wanafunzi kuelezea maana ya vina, ubeti, mishororo, mizani na

kibwagizo

Aidha bahari za mashairi

Tathmini: km uk 205-206

Mwongozo uk 200-201

**Kuandika: mtungo**

**Kuandika: mtungo**

Mwalimu awape wanafunzi imla ya maneno yenye sauti s na z

Mwalimu awakumbushe wanafunzikuhusu maendelezo ya maneno na uakifishaji

Wanafunzi wakumbushwe jinsi ya kujaza mapengo au vihasho ili mtungo uwe na mtiririko ufaao

Aidha wanafunzi wahimizwe kuchagua viteuzi vifaavyo zaidi

Tathmini: km uk 206

Mwongozo uk 200-201

## SURA YA KUMI

**Kusoma: ufahamu**

Sungura kizimbani (sehemu ya pili)

Uchambuzi wa picha

Kuhusisha wanafunzi kusoma ufahamu zaidi ya mara moja na kwa kiada

Mwalimu auchambue ufahamu na kueleza ujumbe ulio katika ufahamu

Kuorodhesha msamiati na kutungia sentensi ukitumia baadhi ya msamiati huo

Tathmini: km uk 208-210

Mwongozo 201-203

**Sarufi**

**Vivumishi**

Kivumishi ni neon linaloelezea habari ya mtu au kitu jinsi kinavyoonekana au kinavyofikiriwa

Vivumishi hutoa habari zaidi kuhusu nomino

Mwalimu apeane imla kuhusu sauti gh na h

Wanafunzi wahusishwe katika kutaja vivumishi vya idadi, sifa na pekee

Wanafunzi wahusishwe katika kutunga sentensi zenye vivumishi kwa umoja na wingi

Vilevile wataje vivumishi wakizingatia ngeliainati

Tathmini: km uk 210

Mwongozo uk 203

Kurunzi uk 13

**Matumizi ya lugha:**

**Mimea na matunda**

Mwalimu atangulize kwa imla ya sentensi zenye vitate

Mwalimu awaulize wanafunzi wataje mimea ambayo wanafahamu na mazao yake

Mwalimu awakumbushe wanafunzi yale ambayo walijifunza hapo awali kuhusu mimea na mazao

Wanafunzi waelekezwe kuisoma mifano mbalimbali

Aidha wahusishwe kutunga sentensi mbalimbali zinazohusiana na mimea na matunda

Tathmini: km uk 211

Mwongozo uk 19-20

Kkd uk 34-35

Novels,Updated ICT,KASNEB,College,High School,Primary Notes &Revision Kits 0714497530

**Sarufi**

**Nomino kutokana na vitenzi**

Kutanguliza kwa imla ya maneno ya gh na h

Mwalimu atoe mifano ya nomino kutokana na vitenzi kama vile:

- Kitenzi nomino
- Soma msomaji
- Imba mwimbaji
- Shone mshonaji
- Saka msasi
- Jenga mjenzi
- Linda mlinzi

Wanafunzi waelekezwe kusoma mifano mbalimbali

Wanafunzi watunge nomino kutokana na vitenzi

Vilevile watunge sentensi mbalimbali

Tathmini: km uk 210-211

Mwongozo uk 203

Kkd uk 106

Kusoma na kuandika

Hadithi: yohana mtiifu

Mwalimu awahusishe wanafunzi katika kuandika imla ya maneno yenye sauti ch n ash

Wanafunzi wakumbushwe kuhusu usomaji kv. Kutotumia vidole, kufuata uakifishaji, kusoma kwa utaratibu ufaao

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma hadithi na hatimaye wayajibu maswali

Tathmini: km uk 212-213

Mwongozo uk 206

Mazoezi ya ziada: km uk 214-218

## INSHA MUHULA WA TATU

### BARUA YA KIRAFIKI

Pia huitwa ya kirafiki

Hutumiwa watu wa ukoo au familia au marafiki wenye uhusiano wa karibu

Huwa na sehemu nne kuu

- Anwani
- Maamkizi
- Mwili/ kiwiliwili
- Hitimisho

### Anwani

- Huwa na jina la mwandishi,
- jina la shule ya mwandishi
- Sanduku la posta
- Mji na tarehe

### Maamkizi

- Huwa na mwanzo maalum

- Mfano: kwa mpendwa nina
- Kwa laazizi kimani

**Mwili**

- Hulenga lengo maalum
- Hutangulizwa  kwa salamu
- Lugha rasmi haitumiwi
- Mambo mengi huchopekwa ndani

**Hitimisho**

- Huhitimishwa kwa kumtaja mwandishi

**Mfano**

| |
|---|
| KAMAU MWANGI<br><br>S.L.P<br><br>MJI<br><br><br>TAREHE |

| |
|---|
| KWA MPENDWA BABA, |

| |
|---|
| MWILI |

| |
|---|
| NI MIMI MWANAO WA PEKEE<br><br>IBRAHIM MPOTE |

**MSAMIATI**

Pokea salamu sufufu

Tumbitumbi

Nyingi kama wana wa ibrahimu

Nyota angani

Mchanga baharini

Nywele kichwani

Mimi ni mzima kama kigongo

Imara kama chuma cha pua

Chanda chema huvikwa pete

Subira huvuta heri

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

Mchelea mwana kulia hulia yeye

Mchumia juani hulia uvulini

Majuto ni mjukuu

Furaha mpwitompwito

Furahi ghaya

## FAIDA ZA MITI

Mti ni mmea

Mti mdogo ni mche/ miche

Hutokana na mbegu- huota

Miti mingi pamoja na msitu

Miti ina faida sufufu:

- Hutupa mbao za ujenzi
- Kuni na makaa
- Huzuia mmomonyoko wa udongo
- Hutupa matunda
- Kivuli wakati wa kiangazi
- Hukinga upepo mkali
- Hutumiwa kwa kutengeneza nyua
- Hurembesha mandhari
- Huwapa wadudu chakula na nyuni
- Huvuta mvua
- Huwa ni makao ya wanyama hasa pori
- Kivuto cha watalii ambao huleta pesa za kigeni
- Husafisha hewa

## SHEREHE NILIYOHUDHURIA

Sherehe yenyewe

Kuamka na kujitayarisha

Kuamka jogoo la kwanza

Kuamka kabla ya bwana shemshi kupasua matlai

Kuamka alfajiri mbichi

Kudemka demdem, chapua miguu chapuchapu

Kiamshakinywa kitamu ja uki

- Halua kando
- Kilichoniacha nikiramba vidole ovyo

Kukoga kwa maji baridi shadidi

- Baridi barafu kando
- Vuguvugu

Kushtaki uchafu/ kutoa ngongo

Valia mavazi nadhifu

Nguo zilizopigwa pasi na kunyooka twaa maiti kando

Nywele nilizilaza mlazamlaza na kunyooka kama singa ya samba

Kuwaaga wazazi

Kupitia kwa sahibu na kumwita

Kupiga miguu/ kuchapa miguu chapuchapu hadi stani ya magari

Daladala jekundu/ muziki mwanana

Kulipa nauli na kungoa nanga

Kuwasili shereheni

Sherehe yenyewe

Kujiburudisha

Kuvudi nyumbani

Kusimulia na kulala

# UMUHIMU WA MAJI

Maana ya maji

Kiowevu kinachopatikana kwenye mito, maziwa, bahari kinachotokana na mvua

Maji yana faida sufufu/ telele/ tolatola/ chungu nzima kwa adinasi, hayawani na mimea

Baadhi ya faida ni:-

Hutumika kwa upishi wa vyakula na vinywaji ainati

Usafiri majini – vyombo kama:

Motoboti

Mashua

Ngalawa

Nyambizi

Merikebu

Usafi wa mwili mazingira na mavazi

Huuzima moto unapochipuka na kuteketeza meli

Ni makao ya wanyama kv. Samaki, viboko, mamba

Michezoni kv. Kupiga mbizi

Huchemshwa na kunywewa kukunga roho

Kunyunyizia mimea- ukame/ uhaba wa maji

Huzungusha mashine na mitambo kutoa nguvu za umeme

Kupoza injini zinakuwa moto zaidi

Huchanganya kemikali shambani

Usafi wa mazingira kwa jumla

**Msamiati**

Nishati au nguvu za umeme

Kububunjika kwa maji

Maradhi tumbitumbi kama kipindupindu huzuiwa kwa kuzuia yakitumika ipasavyo

Mizigo mizito kama nanga

Shehena za mizigo

Mchafu kama fuko

Kusteri na kunawili

Hamamu na madibwi

**Methali**

Maji hufuata mkondo

Mkamia maji hayanywi

Mfa maji haachi kutapatapa

Maji ni uhai

**MOTO**

Chanzo

Wakati upi

Jadili ulikuwa wapi na ulijuaje

Moto shuleni

Ilikuwa alfajiri na mapema

Alfajiri mbichi

Usiku wa manane

Vimulimuli vya moto, moshi, mwangaza

Usingizi wa pono

Mtihani siku iliyofuata

Niligutuka/ kushtuka kama jinni

Niliamshwa na nyende za jkutisha

Ndimi za moto zilitafguna mapaa ya bweni letu

Moto ule ulitafuna paa na kumeza bila huruma

Moto ule ule ulitafuna paa na kumeza bila huruma

Patwa na woga, jitabawalia , jinyea

Banana mlangoni bila tumaini/ piga sala

Pata mwanya na kuponyoka, fyatuka kama risasi

Piga unyende ungewaamsha wafu

Piga simu, ita, omba msaada

Wanakijiji kufika

Zimamoto na ambulensi

Msalaba mwekundu

Wanafunzi kuzirai

Wengine kuteketea hadi hawangetambulika

Ufuoni/ mochari

Nodi

Wanahabari

Kusimulia

Alfajiri kufika

Mbwa kubweka kwa huzuniutafiti kuanza

**Msamiati**

Mlipuko wa petrol

Harufu kuhanikiza hewa

Piga unyende/ usiahi/ kamsa

Mbio kama swara

Meza mrututu wa mate machungu

Dodokwa na machozi njia mbilimbili

Midomo ilinitetema na mikono haikuinulika

Piga kamsa wingu lililokuwa limefunga likaanza kuondoka kodogokidogo

Nilipiga kamsa upepo ukasita kuvuma

**Methali**

Ajali haina kinga wala kafara

Ajali haijali

Majuto ni mjukuu

Mbio za sakafuni huishia ukingoni

Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe